SportPesa
TZS. 918,137,180
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 2

## KESI YA MBOWE

Shahidi: Niliyafanyia kazi maneno ya kusikia kufungua kesi ya ugaidi


KUELEKEA UCHAGUZI KENYA...
Raila aendelea kubaki 'mtoto wa Baba' - Rais Kenyatta
Ukurasa 13
Ukurasa 14
siasa
JUMATANO FEBRUARI 9, 2022
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
WAZIRI MKUU BORISS JOHNSON UINGEREZA WAAMSHA 'DUDE', KISA MISURURU YA TAFRIJA 'HARAMU'
MIAKA 45 CCM
Chama kinakwenda na wakati, lakini kinabanwa
•Ni hofu kuogopa nguvu ya soko, ubinafsishaji
Na Ani Jozeni
KUTAFAKARI njia iliyofuatwa au inayofuatwa na Chama Cha Mapinduzi miaka 45 baada ya chama hicho kuundwa Februari 5, 1977 ni jambo lenye mapana na marefu tofauti, kulingana na kila anayefanya uchambuzi huo.
Kwanza kuna upeo wa kukiangalia chama, kwani kila mmoja anakuwa na hisia chanya zaidi kuhusu kipindi alichoifahamu CCM, halafu alinganishe na yaliyotokea baadaye, inamaanisha kuwa vizazi tofauti vina sura tofauti za chama, na hisia mbalimbali au uthabiti, maadili ya uongozi katika kipindi kilichopita hivyo, hakuna njia ya 'kusawazisha' taswira hizo.
Wakati chama kinaadhimisha miaka 45, kitakachoangaliwa siyo yaliyopita au kulitokea nini ila makada, wanachama na jamii...
nje, mabenki, bima, umeme na uendeshaji bandari, serikalini waliona shughuli hizo sasa zitasimamiwa na wazawa.
Tafsiri hiyo ya Ujamaa na Kujitegemea isiyo rasmi na inayoeleweka kisaikolojia kwa wengi inaendelea kuwa kati ya ishara chanya, hasa katika kukubaliana hata ikabaki katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuwa Tanzania ni nchi inayofuata siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.
Itakumbukwa kuna wakati Miiko ya Uongozi (kutoshiriki shughuli yoyote ya kibepari, yaani kutafuta fedha kibiashara, nje ya mshahara, kwa uwekezaji na kuwaajiri wengine) iliondolewa mwaka 1991 kwa 'Azimio la Zanzibar' au Tangazo la Zanzibar.
Inawezekana wapo baadhi ndani ya jamii wawe wanasiasa au wengineo kuna yanayowachanganya ndani ya mageuzi hayo. Kwa mfano dhana 'kukopa na kuwa na deni kubwa la taifa kutasababisha nchi kupigwa mnada.'
Tatizo la kuogopa nguvu ya soko na masuala ya ubinafsishaji pamoja na uwekezaji wa kigeni ni mtihani ambao siyo rahisi sana, hata hivyo uchumi kitaifa unaenda mbele pale kunakuwapo mazingira huru, hakuna ubaguzi wa nani ana uwezo wa kuza au...

UKURASA 11

Nipashe
Jumatano Februari 9, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580851
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 4

### HAMAD AJITOA ACT AKITOA TUHUMA KIBAO

ALIEYEKUWA Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo Hamad Masoud Hamad, ametangaza kujiondoa katika chama hicho...

UKURASA WA 19

### BUNGE LATOA MBINU UDHIBITI UTAKATISHAJI

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeitaka serikali kutunga sera, mbinu na mifumo ya utakatishaji wa fedha haramu, ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji Fedha...

## Samia awapa siku 90 ma-RC anwani makazi

UKURASA 3



Paul Makonda

# Mahakama yabariki Makonda asakwe

UKURASA 2



UKURASA 4

Maofisa wa Jeshi la Polisi wanaotuhumiwa kwa kesi ya mauaji ya mfanyabiashara Musa Hamis (waliokaa mstari wa mbele), wakiwa kwenye chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Mtwara, wakati kesi inayowakabili ilipotajwa jana. **PICHA: ABDALLAH KHAMIS**

# Ulinzi mkali, mvutano polisi wakipandishwa kizimbani

Form 281d

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

**Advertisement of Winding-up Petition**
**Pursuant to Rule 99(1) of the Companies (insolvency) Rules 2005**
**Misc. Commercial Case No.42 of 2021**

IN THE MATTER OF: BAHDELA CO. LIMITED

A Petition to wind up the above-named Company of:

Address: The Registered office of the Company is at Plot No.186053/23, Upanga Street, P. O. Box 5950, Dar es Salaam, Tanzania.

presented on: 31ST AUGUST, 2021

by: (name and address of petitioner) PETROFUEL (T) LIMITED OF P.O.BOX 14525, PLOT NO.33/1 & 34/1, MBAGALA INDUSTRIAL AREA, DAR ES SALAAM, TANZANIA

Claiming to be a [creditor] of the Company, is fixed for orders at (Name of Court) THE HIGH COURT OF TANZANIA, COMMERCIAL DIVISION AT DAR ES SALAAM

on (date): 10TH MARCH 2022

at (time): 9:00AM IN THE MORNING
(or as soon thereafter as the petition can be heard)

Any person intending to appear on the hearing of the Petition (whether to support it or to oppose it) must give notice of his intention to do so to the petitioner or his/its Advocate in accordance with Rule 104(1) of the Companies (Insolvency) Rules 2005 by 16:00 hours on the business day before the date of the hearing given above.

The Petitioner's Advocate is: S. Ishengoma, SA Law Chambers, Advocates, PPF Tower, 4th Floor, Ohio /Garden Avenue Street, P.O. Box 22691, Dar es Salaam
Mobile: 0786222242
Email: adv.ishengoma@gmail.com, s.ishengoma@salawchambers.co.tz
(REF: SI/108/PFL)

**Dated 8th February, 2022.**

216697102

MICHEZO SIMBA KUTOA MAKUCHA KWA ASEC MIMOSAS CAF UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Katiba na Sheria, George Simbachawene (katikati), akizungumza katika kikao cha kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara yake ya Mwaka 2021/2022 kwa kipindi cha nusu mwaka Julai hadi Desemba 2021, jijini Dodoma, jana. **PICHA: WKS**

# Mahakama yabariki Makonda asakwe

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Dar es Salaam imetoa amri ya kutangazwa magazetini nyumba aliyokuwa anaishi Masaki na kijijini kwao, Kolomije mkoani Mwanza, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda.

Lengo ni kuhakikisha Makonda anapata taarifa ya uwapo wa maombi ya kufungua kesi ya jinai katika mahakama hiyo yaliyofunguliwa na mwandishi wa habari mwandamizi, Saed Kubenea.

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Aron Lyamuya, baada ya mawakili wa Kubenea; Nyaronyo Kicheere na Hekima Mwasipu, kuiomba mahakama hiyo kutoa samasi ya kutangazwa maeneo mbalimbali.

Mawakili hao walidai wamemtafuta maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam, yakiwamo makazi yake ya Masaki aliyoishi wakati akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na kumpigia simu yake ya mkononi bila mafanikio.

"Tumekwenda kule kwake Masaki alikokuwa akiishi, tumeambiwa amehama. Vilevile, tumepata mawasiliano yake ya simu ya Airtel 0682009009, hapatikani," alidai Kicheere.

Wakili huyo aliendelea kudai: "Kutokana na hilo, tunaiomba mahakama itupatie samasi ya kumtangaza maeneo saba, ili aweze kupata taarifa ya kesi iliyoko hapa kwani ni haki yake kupata taarifa."

Aliyataja baadhi ya maeneo hayo, akitamka: "Tutapeleka pale alipokuwa anafanya kazi kwa mara ya mwisho kwa maana Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam; nyumba aliyokuwa anaishi mara ya mwisho na tutatangaza gazetini."

Maeneo mengine ni pamoja na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Saalam. Wakili Kicheere alifafanua kusudio lao hilo akidai: "Ili kama anasafiri aweze kuona na au watakaokuwapo wanaweza kumwonyesha.

"Lakini tutapeleka bandarini ili kama anakwenda kupunga upepo Unguja, aone na kijiji alikozaliwa cha Kolomije, Misungwi mkoani Mwanza."

Baada ya kuwasilishwa kwa hoja hiyo, Hakimu Mkazi Lyamuya alimuuliza Wakili wa Serikali, Deisy Makakala, kama ana chochote cha kuieleza mahakama, wakili huyo akidai:

"Nimesikiliza hoja za wakili msomi ila zinaelekezwa kwa mjibu maombi namba tatu (Makonda) na mimi nimesema ninamwakilisha DPP na DCI. Kwa hiyo, ninafungwa kumzungumzia mjibu maombi namba tatu." Baada ya Deisy kutoa maelezo hayo, Wakili Kicheere alinyanyuka na kudai: "Ninamshukuru sana wakili msomi wa serikali" kisha Hakimu Lyamuya akatamka kwamba amesikiliza maombi ya waleta maombi, lakini akawa na angalizo, alisema:

"Kweli tukabandike Airport (uwanja wa ndege), bandarini! Hilo ni kosa, tunaweza kushtakiwa kwa uchafuzi wa mazingira lakini kama ni gazetini, nyumba aliyokuwa anaishi hapo sawa."

Hata hivyo, Wakili Kicheere alinyanyuka na kumwomba hakimu kuelezea kwamba pamoja na maeneo mengine kwa mujibu wa sheria, iwe kijijini kwao, huko nako wapeleke, ikabandikwe kwenye zizi la ng'ombe au kwenye mti unaoweza kumfanya kuonekana.

Akihitimisha maombi hayo, Hakimu Lyamuya alisema: "Maeneo yatakayoruhusiwa ni magazeti ya ndani, moja la Kingereza na lingine la Kiswahili ambalo linasambaa nchi nzima, nyumba aliyokuwa akiishi na nyumbani kwao Kolomije."

Baada ya kutolewa kwa uamuzi huo wa mahakama, Wakili wa Serikali, Deisy aliiomba mahakama iwapatie siku 21 wajibu maombi namba moja na namba mbili yaani Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na mahakama ilikubali na kuiahirisha kesi hiyo hadi Machi 2, mwaka huu saa 5:00 asubuhi.

Maombi hayo ni ya kesi ya jinai iliyosajiliwa mahakamani huko kama Miscellaneous Criminal Application Na. 1 ya mwaka 2022 na Kubenea anayemtuhumu Makonda kwa makosa mbalimbali.

Mbali na Makonda, wengine kwenye kesi hiyo ni DCI na DPP ambao wanadaiwa wameshindwa kuchukua hatua za kumfungulia mashtaka ya jinai mtuhumiwa huyo.

Miongoni mwa makosa hayo anayotuhumiwa kuyafanya Makonda ni matumizi mabaya ya madaraka ya umma wakati akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kuvamia Kituo cha Televisheni cha Clouds na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, Makonda anadaiwa siku ya Machi 17, 2017, akiwa na watu waliobeba silaha za moto, alivamia Clouds TV na kumwagiza mtangazaji wa kipindi cha Shilawadu kurusha video inayomwonyesha mwanamke aliyejulikana kwa jina la Grace.

Inadaiwa kuwa katika video hiyo, ambayo haijulikani aliyeandaa, mwanamke huyo alidaiwa kuonekana akifanya tendo la ndoa na Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima.

## KESI YA MBOWE

# 'Niliyafanyia kazi maneno ya kusikia kufungua kesi ugaidi'

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa 13 upande wa Jamhuri, Inspekta Tumaini Swila, ameligusa shtaka la kula njama kuchoma masoko na kulipua mikusanyiko ya watu baada ya kukiri kwamba katika maelezo yake, maelezo ya ACP Ramadhani Kingai, SP Jumanne na Luteni Urio, hakuna sehemu waliyosema washtakiwa watafanya hayo.

Inspekta Swila amekiri kwamba alifanyia kazi maneno ya kusikia kwa Kamishna wa Polisi Robert Boaz aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), akafungua jalada la kesi ya ugaidi bila ya kuwa na maelezo ya mlalamikaji huyo (Boaz).

Shahidi alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga wakati akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibata katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu.

Alidai alichukua sampuli nne za mshtakiwa Halfani Bwire kupeleka kwenye uchunguzi kwa maelekezo ya Afande Kingai.

Shahidi huyo alidai alisomea mchakato wa uchukuaji wa sampuli katika Chuo cha Taaluma ya Polisi lakini yeye si mchunguzi.

Alidai kuwa nyumbani kwa Bwire, walichukua sampuli ya notebook lakini Kingai hafahamu na aliikabidhi kwa Sajenti Johnson kwa utaratibu wa kipolisi.

Wakili Kibatala alihoji akitaka kujua michoro ya ramani katika notebook ya Bwire aliichora kabla ya kukutana na Luteni Urio na Mbowe au la, shahidi akidai kwake hilo halikuwa muhimu kwa kuwa jambo la msingi kwake lilikuwa kujua mwandiko ni wa nani.

Alidai kidaftari hicho hakitakuwa muhimu kwenye kesi hiyo ya ugaidi kama mshtakiwa Bwire alichora michoro hiyo Mei 5, mwaka 2020.

Akiendelea kuhojiwa, shahidi huyo alidai alifungua jalada la kesi Julai 18, mwaka 2020, kabla hajamhoji Kamishna Boaz ambaye alihojiwa Oktoba 13, 2020 ikiwa ni baada ya miezi mitatu baada ya jalada kufunguliwa. Inspekta Swila alidai hakuwapo wakati Luteni Urio anatoa taarifa za ugaidi kwa Kamishna Boaz na alikiri kuwa alifanyia kazi maneno ya kusikia kutoka kwa Boaz.

Alidai alifungua jalada akiwa na taarifa ya kesi ya ugaidi ambayo alipokea kutoka kwa Kamishna Boaz.

Alipohojiwa sababu za kufungua kesi kabla ya kuchukua maelezo ya mlalamikaji, shahidi huyo alidai ikiwa kesi imefunguliwa na raia, lazima maelezo yachukuliwe kwa haraka lakini kama ni polisi, maelezo sio lazima yachukuliwe kwa haraka.

Wakili Kibatala akataka shahidi aonyeshe ni kifungu gani katika Mwongozo wa Jeshi la Polisi (PGO) kinaonyesha tofauti hiyo.

Shahidi alipewa PGO asome eneo hilo, lakini alidai hakumbuki lakini alisoma eneo lingine ambalo mwongozo unamtaka polisi aliyepokea taarifa kuandika maelezo ya mtoa taarifa yoyote.

Inspekta Swila alidai hoja ya Kibatala kwamba walimkamata Luteni Urio na wakampiga baada ya kutajwa na mshtakiwa wa pili, Adamu Kasekwa maarufu Adamoo kisha wakampa dili la kuwa shahidi, si ya kweli.

Alidai kuwa wakati anafungua jalada la uchunguzi, Afande Kingai hakumwambia kwamba kuna tuhuma za ugaidi na si yeye aliyeamua kufungua jalada la kesi ya ugaidi.

Wakili Kibataka alimpa maelezo ya wapelelezi wenzake aonyeshe sehemu waliyosema washtakiwa watachoma masoko na kulipua mikusanyiko ya watu. Akijibu hoja hiyo, shahidi huyo alidai katika maelezo ya Afande Kingai na Luteni Urio hakuna sehemu ambayo wamesema washtakiwa watachoma masoko.

Alidai kuwa katika maelezo ya Afande Jumanne, hakuna sehemu inayosema watachoma masoko na katika maelezo yake, hakuna sehemu aliyoandika kwamba washtakiwa watalipua mikusanyiko ya watu.

Inspekta Swila alidai kuwa baada ya kufungua jalada la kesi, DCI Boaz alimtaka kuwa mpelelezi katika shauri hilo la ugaidi na alichukua maelezo mbalimbali ikiwamo maelezo ya Luteni Urio.

Alidai hakuna mahali kulikoandikwa alikuwa msaidizi wa Afande Kingai ama Kingai kushirikiana naye katika kufanya upelelezi.

Akizungumzia bastola inayodaiwa alikamatwa nayo mshtakiwa Adamu Kasekwa kule Moshi aina ya Luger yenye namba A5340, shahidi huyo alidai hakuwahi kuitambua kwa maneno CZ100 CALLBRE kutoka mdomoni kwake.

Awali akihojiwa na Wakili Fredrick Kihwelo, shahidi alidai kiongozi aliyetaka kudhuriwa ni aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, na hawajui viongozi wengine waliotaka kudhuriwa.

Shahidi huyo alidai kufanya maandamano sio kosa kama utaratibu ukifuatwa lakini kwa upande wa kesi hiyo washtakiwa ndio wanajua kama walipanga kufanya maandamano.

Washtakiwa katika shauri hilo ni Mbowe, Bwire, Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanadaiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi ikiwamo kulipua vituo vya mafuta, mikusanyiko ya watu, kuchoma masoko na kuwadhuru viongozi wa serikali kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020.

HABARI KITAIFA

# Sababu kushuka mfumuko wa bei

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MFUMUKO wa bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Januari, 2022 umepungua hadi asilimia 4.0 kutoka asilimia 4.2 kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba, 2021 huku bidhaa za mavazi zikichangia hali hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii, Ruth Minja, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya mfumuko wa bei kwa waandishi wa habari.

"Kupungua kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Januari, 2022 kumechangiwa hasa na kupungua kwa mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za vyakula kwa kipindi cha mwaka ulioishia mwezi Januari ,2022 ikilinganishwa na kipndi cha mwaka ulioishia mwezi Desemba, 2021," alisema.

Aidha, alisema mfumuko wa bei ambao haujumuishi bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwezi Januari, 2022 umepungua hadi asilimia 3.1 kutoka asilimia 3.9 ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba 2021.

Kadhalika, alisema mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula visivyochakatwa, nishati na bili za maji kwa mwezi Januari 2022 umepungua hadi asilimia 3.3 kutoka asilimia 4.6 ilivyokuwa mwezi Desemba, 2021.

"Vilevile baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizoonyesha kupungua kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Januari 2022 ikilinganishwa na mwaka ulioishia mwezi Desemba 2021 ni mavazi kutoka asilimia 4.5 hadi asilimia 2.8, viatu kutoka asilimia 4.6 hadi asilimia 4.4, kodi ya pango asilimia 4.2 hadi asilimia 1.5."

"Magodoro kutoka asilimia 12.3 hadi 7.3, majokofu kutoka asilimia 4.2 hadi asailimia 1.5, cherehani kutoka asilimia 9.1 hadi asilimia 5.0, simu janja kutoka asilimia 3.5 hadi aasilimia 3.3, vyombo vya nyumbani kama sahani kutoka asilimia 16.7 hadi asilimia 3.6. Luninga kutoka asilimia 3.5 hadi asilimia 1.2 na malazi kwenye hoteli na nyumba za kulala wageni kutoka asilimia 6.6 hadi asailimia 2.9," alisema.

Alisema hali ya mfumuko kwa baadhi ya nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka ulioishia mwezi Januari 2022 nchini Uganda mfumuko wa bei kwa

mwaka ulioishia mwezi Januari 2022 umepungua hadi asilimia 2.7 kwa mwaka ulioishia Desemba 2021.

Alieleza kwa upande wa Kenya mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Januari 2022 umepungua hadi asilimia 5.39 kutoka asilimia 5.73 kwa mwaka ulioishia Desemba 2021.




Rais Samia Suluhu Hassan akishuhudia Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akipokea kwa niaba yake, bango lenye anwani ya makazi ya Ofisi ya Rais, Ikulu kutoka kwa Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, baada ya kuzungumza katika kikao kazi cha wakuu wa mikoa kuhusu mfumo wa anwani za makazi, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Samia awapa siku 90 ma-RC anwani makazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametoa miezi mitatu kwa Wakuu wa Mikoa kukamilisha utekelezaji wa mfumo wa anuani za makazi postikodi, huku akionya ubadhirifu wa fedha za mradi huo.

Aidha, amesema kutokana na fedha za mradi kushuka kutoka Sh. Bilioni 720 hadi 28 serikali imeamua kuacha kutumia makandarasi.

Pamoja na hayo, ametaja faida za kuwapo kwa mfumo huo ikiwamo ulinzi na usalama na kumtambua kila mtu anayefanya biashara mtandaoni na watapaswa kulipa kodi ipasavyo.

Samia aliyasema jana jijini hapa katika kikao kazi cha Wakuu wa Mikoa kuhusu utekelezaji wa mfumo huo.

"Kazi hii ifanyike kama oparesheni maalumu katika muda uliopangwa (Mei) na kushirikisha wananchi kikamilifu kama ilivyofanyika kwenye ujenzi wa madarasa,"alisema.

Rais Samia alisema itakapofika Mei iwapo kuna Mkuu wa Mkoa utekelezaji haujafanyika vizuri atakaa naye ana kwa ana.

"Kama unapata changamoto wakati unatekeleza ni vyema kusema mapema ili tukusaidie ziondoke uendelee na zoezi, lakini ukikaa na changamoto zako hadi mwisho na ukashindwa kutekeleza itabidi tukaa ana kwa ana kuelezana," alisema.

Alibainisha kuwa mradi huo ni operesheni maalumu ambayo ataisimamia mwenyewe kwa kusaidiwa na Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kwa pande zote mbili za Muungano.

Alisema mradi huo unapaswa kukamilika mapema ili kufanikisha sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti, mwaka huu ili kufanyika kwa ufanisi.

"Sensa hii itategemea zoezi hili kumalizika, likimalizika kwa ufanisi litasaidia sensa kufanyika kwa ufanisi, kama kuna nyumba ilirukwa hawakuhojiwa itaonesha, na waliopewa eneo hilo itabidi warudie kufanya, sensa kuhesabu watu ni siku moja lakini hadi mahesabu yatoke ni miezi kadhaa, kwa hiyo kumrudisha mtu kuhoji tena sio kitu cha ajabu, Mfumo huo utasaidia kutopika taarifa na kupata idadi halisi ya watanzania," alisema,

Hata hivyo, alisema mradi huo awali ulipangwa kugharimu Sh. bilioni 720 na kwasasa utatekelezwa kwa Sh. bilioni 28 na fedha hizo zitapelekwa kwenye Mikoa kulingana na ukubwa wa eneo.

"Fedha hii sio OC(matumizi ya ofisi), fedha hii ni ya mradi, OC mtaendelea kutumia OC zenu mlizonazo, unakwenda kuhamasisha tumia OC yako fedha hii iende kwenye mradi na katika mradi huu kulikuwa na michango ya Halmashauri zichange kwa zile gharama za lazima, tujitahidi sana kutumia nyenzo zilizopo,"alisema.

Alisema kuna fedha nyingi Halmashauri zinaliwa.

"Nimetoka Mara jana (juzi) fedha zinakung'utwa tu bila kujali maendeleo ya wananchi twende tukazibane Halmashauri zikatoe," alisema.

Aliagiza Wizara ya Fedha kuhakikisha fedha zilizotengwa zinatoka kwa wakati na pia fedha za kurahisisha mfumo wa kidigitali ndani ya mfumo wa serikali ikiwamo mkongo wa taifa ufike kila Wilaya zitolewe.

Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Sulemani Abdullah, alisema wako tayari na imara kufanikisha mradi huo muhimu kwa taifa.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema: "Jambo lingine Mheshimiwa Rais ni kwamba kiasi ambacho kingetakiwa kutumika katika mradi huu awali ilikuwa imeshauriwa na wataalamu kuwa ni Sh. bilioni 720, lakini kwa kushirikisha wananchi na kutumia wataalamu wetu imeshuka hadi Sh. bilion 28, hivyo kuokoa kiasi cha Sh. bilioni 668."

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema Tamisemi imekuwa ikitoa maelekezo mbalimbali kwa mamlaka za mikoa kutunga sheria ndogo pamoja na kuandaa ramani za kiutawala.

Katibu Mkuu Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonazi, alisema kukamilika kwa mradi huo kutaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kwa ukanda wa Afrika Mashariki ambayo maeneo yake yote yanafika kwa kutumia anuani za makazi.

Kamisaa wa Sensa, Spika Mstaafu, Anne Makinda, alisema kukamilika kwa mradi huo wa anuani za makazi kutasaidia kuwezesha sensa kufanyika kikamilifu na kwa mara ya kwanza watahesabiwa watu na makazi yao.

# Ulinzi mkali, mvutano polisi wakipandishwa kizimbani

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

KESI ya mauaji inayowakabili maofisa saba wa Jeshi la Polisi mkoani Mtwara, imeahirishwa hadi Februari 22, mwaka huu, itakapokuja kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mtwara, Lugano Kasebele.

Watuhumiwa wa kesi hiyo namba 1 ya mwaka 2022 ni pamoja na mratibu wa polisi Gilbert Kalanje (aliyekuwa OCCID) Wilaya ya Mtwara, Mratibu msaidizi wa polisi, Charles Onyango (aliyekuwa OCS) kituo cha polisi Mtwara na Mratibu wa Polisi Msaidizi, Nicholaus Kisinza (aliyekuwa Mkuu wa Intelijensia ya Jinai Mkoa wa Mtwara).

Wengine ni Mkaguzi wa Polisi, John Msuya (aliyekuwa mganga mkuu zahanati ya polisi Mtwara), Mkaguzi wa Polisi Msaidizi, Marco Mbuta, Mkaguzi wa Polisi Shirazi Mkupa na Koplo Salimu Juma Mbalu.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kula njama na kisha kumuua mfanyabiashara wa madini, Musa Hamis, Januari 5, mwaka huu na kwenda kuutupa mwili wake katika Kijiji cha Hiari, Wilaya ya Mtwara.

Kwa mara ya kwanza watuhumiwa hao walifikishwa mahakamini Januari 15, mwaka huu, baada ya kukamatwa na kuhojiwa katika vituo mbalimbali vya polisi kati ya Januari 22 na 24, mwaka huu.

Musa anadaiwa kukumbana na kadhia hiyo ya mauaji wakati akidai fedha zaidi ya Sh. milioni 33.7 zilizochukuliwa na maofisa hao baada ya kumkamata Oktoba 20, mwaka jana akiwa kwenye nyumba ya kulala wageni ya Sadina iliyoko mkoani Mtwara.

**NJE YA MAHAKAMA**

Watuhumiwa katika kesi hiyo walifikishwa mahakamani majira ya saa 3:19 asubuhi chini ya ulinzi mkali wa polisi, wakishushwa nyuma ya jengo la mahakama.

Kabla ya kushuka kwenye gari lililowapeleka mahakamani, watuhumiwa hao walionekana wakifunikwa sura na baadhi ya askari waliokuwa wamevaa kiraia.

Hata hivyo, Gilbert Kalanje, mmoja wa watuhumiwa hao na aliyekuwa Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Mtwara, aliposhuka kwenye gari, aliwataka askari wenzake wasiwazuie waandishi kupiga picha.

"Waacheni wapige picha, waacheni wapige picha, wanafanya kazi yao, pigeni pigeni mpaka mtosheke," alisikika Kalanje akitamka wakati akiingia kwenye chumba cha mahakama.

Baada ya watuhumiwa kuingia, askari wawili walizuia mlango na kuwataka waandishi wasiingie ndani, hali iliyozua mabishano ya muda baina ya askari na waandishi wa habari.

Hakimu mkazi mfawidhi Kasebele baada ya kupewa taarifa kuhusu mabishano hayo, waandishi wa habari waliruhusiwa kupiga picha na kisha askari kuwaamuru watoke nje ya chumba cha mahakama kwa maelezo kuwa nafasi ni ndogo ndani ya chumba hicho.



Mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kinyali (kulia), akipokea sehemu ya miche ya matunda kutoka kwa Ofisa Mradi wa Inades Formation Tanzania, Fortunata Tarimo, kwa niaba ya klabu ya wanafunzi ya ustawi wa punda ya shule hiyo, katika kata ya Migoli, wilayani Iringa mkoani Iringa jana. Shirika la Inades limegawa miche ya miti mbalimbali ikiwamo ya matunda kwa shule za msingi ambazo zipo kwenye mradi wa ustawi punda na kuboresha maisha ili kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi unaotekelezwa katika vijiji vya kata hiyo. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## Rais leo kuzindua barabara za mzunguko

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajia kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara za mzunguko (Ring roads) zenye urefu wa kilomita 112.3 zitakazojengwa katika Jiji la Dodoma ili kupunguza msongamano wa magari.

Barabara hizo ujenzi wake unagharimu zaidi ya Sh. bilioni 221 na zinatarajiwa kukamilika mwaka 2025.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema jana kuwa hafla hiyo itafanyika eneo la Makutopora na kuwataka wananchi kujitokeza kwa wingi.

"Barabara hii ni kiungo muhimu na barabara nyingine za Jiji la Dodoma ikiwa imegawanya kwa makandarasi wawili kutoka China, mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2025," alisema.

Aidha, alisema mkoa huo kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) imepanga kuboresha barabara zote za ndani ili zipitike kwa urahisi.

"Wananchi mjitokeze kwa wingi na itasaidia kutambua fursa zinazoambatana na ujenzi huu, niwaalike kwenye mkutano huu mkubwa ambao Rais atazindua ujenzi wake, barabara hizi zitafanya mandhari ya Jiji la Dodoma kuwa tofauti na kuvutia," alisema.

Alisema barabara hizo zitaifungua Dodoma na kuondoa msongamano wa magari ambapo malori makubwa hayatatumia barabara za ndani.

"Mpango wa serikali njia kuu nne za kuingia Dodoma upande wa Iringa, Arusha, Dar es Salaam, Singida zitapanuliwa wapate njia mbili kwa umbali wa kilometa 50 kila upande, kwa kweli masuala ya msongamano hayatakuwapo zikikamilika," alisema.

Alieleza kuwa kwa sasa kuna msongamano baadhi ya barabara lakini sio mkubwa hivyo uamuzi wa kujenga barabara hizo utawaepusha na hali hiyo.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), mkoani humo, Mhandisi Leonard chimago, alisema ujenzi wa barabara hizo ulianza Septemba 2021 na sasa umefikia asilimia nne ya ujenzi.

# Hamad Masoud ajiondoa ACT akitoa tuhuma kibao

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ALIYEKUWA Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo, Hamad Masoud Hamad, ametangaza kujiondoa katika chama hicho.

Hamad ambaye aligombea nafasi ya uenyekiti wa chama hicho taifa na kukosa nafasi hiyo, amefanya uamuzi huo akidai sababu ni chama hakina demokrasia.

Akizungumza jana na waandishi wa habari Mjini Zanzibar, kuhusu uamuzi wake, alisema uchaguzi wa chama hicho uliofanyika hivi karibuni, mkoani Dar es Salaam haukuwa huru na haki.

"Nilichokibaini katika uchaguzi mkuu wa uliofanyika, chama kilikuwa na mgombea wake maalum ambaye kilimuunga mkono," alidai.

Alieleza kuwa katika chaguzi zote za vyama vitatu alivyowahi kuwa mwanachama vya CCM na CUF wajumbe wote wa mkutano mkuu hawakuwa wakimpigia kampeni mgombea maalum badala yake huachiwa kupiga kura kwa mgombea wanayemtaka.

Alidai katika uchaguzi huo wajumbe walilazimishwa kumchagua Juma Duni Haji, na kwamba ni kinyume cha taratibu za uchaguzi.

Hamad licha ya kujitoa katika chama hicho lakini hajaweka msimamo wake kuhusu chama gani atakachojiunga nacho, ingawa kuna taarifa zisizothibitishwa kuwa kuna chama atajiunga nacho.

"Nimeshafuatwa kujiunga na vyama zaidi ya saba, lakini bado sijaamua chama gani nitajiunga," alisema Hamad.

Alidai kuwa awali wapenzi wengi wa Chama cha CUF waliojiunga na ACT - Wazalendo walikuwa na imani kwamba ni chama chenye kuleta mabadiliko, lakini kumbe ni chama cha watu wachache.

Aidha, alisema hakujitoa katika chama hicho kwa sababu ya kukosa nafasi ya uenyekiti, bali ni maamuzi yake baada ya kuona chama hicho hakiendeshwi kwa ukweli na uwazi.

Alisema haoni sababu ya aliyekuwa makamu mwenyekiti Zanzibar Juma Duni Haji kugombea nafasi ya uenyekiti kwa vile nafasi yake ya awali ilikuwa ikimpa nafasi ya kushiriki vikao vyote vya ndani ya chama hicho.

Alisema baadhi ya watu wanaimani kuwa atafilisika kisiasa kutokana na uamuzi wa kujitoa katika chama, lakini anaamini kuwa uamuzi wake huo ni kupiga hatua moja ya kujitangaza kisiasa.

"Japo sijaandika barua rasmi ya kujiengua katika chama, lakini ibaki kuwa kauli yangu hii inatosha kukihama chama hicho," alisema.

Kaimu Naibu Katibu Mkuu ACT-Wazalendo Zanzibar, Salum Bimani, alisema uchaguzi uliofanyika ndani ya chama mwezi uliopita wa kumpata Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ulifanyika kwa huru na haki na kabla ya uchaguzi huo kufanyika ulitoa fursa kwa kila mwanachama kuchukua fomu na kila mgombea kunadi sera zake mbele ya vyombo vya habari.

Alisema ni vyema Hamad akukubali kwamba kura hazikutosha kupata nafasi hiyo dhidi ya mgombea mwenzake Juma Duni Haji na chama kilitoa nafasi kwa mtu kufuata taratibu za kukata rufani kama hakuridhika na matokeo.

Alimpongeza mwanachama huyo kwa kutumia demokrasia yake ya kutoka ndani ya chama na kumtakia safari njema huko aendako.

HABARI KITAIFA

# TCRA yabaini baa jipya la mtandaoni

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema uwezo wa mtandao kuficha utambulisho wa mtumiaji, umewawezesha watu wenye nia ovu kujifanya kama vijana wadogo na kushawishi vijana kuingia kwenye uhusiano wa kimapenzi katika umri mdogo.

Mkurugenzi wa Leseni wa TCRA, John Daffa, alibainisha hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Usalama Mtandaoni 2022 yenye kaulimbiu inayosema 'Pamoja kwa Mtandao Bora'.

Aliwaonya wanaotumia mtandao kuwalaghai vijana hao na kusababisha athari mbalimbali za kiusalama, kuacha mara moja kwa sababu wanaharibu vijana ambao ni taifa la kesho.

Alisema kundi hilo pia linaweza kuiba au kukushawishi uwatumie taarifa yako binafsi kama picha, nywila, mwaka wa kuzaliwa na kuzitumia kufanya uhalifu mtandaoni.

Mkurugenzi huyo alibainisha aina za uhalifu unaofanyika ni kusambaza taarifa za uongo wakilenga kuchafua taswira ya mtu au kufanya manyanyaso na kusababisha usumbufu kwa waathirika wa vitendo hivyo.

Alisema pamoja na mitandao ya kijamii kuwa nyenzo za kulinda usiri, vijana wengi hawatumii nyenzo hiyo na hivyo kusababisha taarifa zao kuonekana kwa watu wenye nia mbaya na hivyo kuzitumia vibaya dhidi yao.

Akitoa takwimu, Daffa alisema kuwa hadi Desemba mwaka jana, idadi ya watumiaji wa mtandao wa intaneti ilikuwa hadi kufikia watu milioni 29.3.

Mkurugenzi huyo alisema Tanzania inaendelea kuwa miongoni mwa nchi ambazo wananchi wake wanapata huduma mbalimbali za mawasiliano kwa gharama nafuu.

Alisema serikali imejipanga vyema kuandaa mazingira bora na wezeshi kwa jamii ya Watanzania kushiriki ipasavyo kwenye uchumi wa kidijitali.

"Tumeshuhudia watu wengi wakiinuka kiuchumi kwa kutumia mtandao. Wengi wanaweza kufanya biashara na kuinua maisha yao wenyewe na wale waliowaajiri ikiwa ni pamoja na kuchangia kwenye Pato la Taifa," Daffa alisema.

Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Connie Francis, alisema Tanzania ni moja ya nchi zilizochukua hatua katika matumizi hayo.

Maadhimisho ya siku hiyo ni mpango wa kimataifa ulioanzishwa mwaka 2004 kwa lengo la kuhamasisha matumizi bora na salama ya mtandao wa intaneti.


TOL Gases Limited | Since 1950 | We Deliver
Plot 4B, Nyerere Road, P.O. Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, E-mail: info@tol-gases.co.tz | sales@tol-gases.co.tz
Website: www.tolgases.com

## TAARIFA KWA UMMA

TOL Gases Limited. 8th February 2022



**MSEMBI LUCAS KIVYELA**

TOL Gases Limited (Tanzania Oxygen) Inapenda kuufahamisha Umma kuwa Bw. Msembi Lucas Kivyela. (Mwenye picha hapo juu) si mfanyakazi wa TOL Gases Limited. hivyo basi Kampuni haitahusika wala kuwajibika na kazi, biashara,ahad au mawasillano yoyote yatakayofanywa na Bw. Msembi Lucas lavyela.

**IMETOLEWA NA:**

**TOL GASES LIMITED**

Directors: M.N Shirima - Chairman (Tanzanian), G. Urasa - (Tanzanian), S. Mponji - (Tanzanian), J. Massawe - (Tanzanian), L.C. Kitoka -TR- URT (Tanzanian), Prof. Abraham Temu - (Tanzanian), Eng. J. Mchange - (Tanzanian)

216695702



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONYESHA NIA: HUDUMA ZA KUSANIFU NA KUKARABATI OFISI**
**KUMBUKUMBU NAMBA. 0010007463**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inaalika taasisi (kampuni) zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kusanifu na kukarabati ofisi kwa ajili ya Maradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, MkoawaTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

Kwa minajiri ya Kujenga uwepo wetu jijini Dar Es Salaam, Kampuni ya EACOP itakuwa inawakaribisha wafanyakazi na wazabuni zaidi ya 300 katika mwaka ujao. Ili kupata ofisi katika wiki zijazo, EACOP inatarajia kuchagua mzabuni atakayesaidia kusanifu na kukarabati eneo la ofisi hiyo kulingana na mahitaji ya kampuni yetu inayokua.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

- Kusanifu, kujenga na kupangilia ukarabati ndani ya eneo lililotengwa.
- Kupata vifaa ndani ya muda kadri inavyohitajika.
- Usanifu na ujenzi wa ndani.
- Upangaji wa nafas iza kukaa.
- Uwezo wa kusimamia kazi husika.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Rekodi inayoonyesha uzoefu wa kutosha katika kusanifu, kujenga na kukarabati ofisi ndani ya jiji la Dar es Salaam kwa kipindi kisichopungua miaka kumi.
- Iwe na uwezo wa kusanifu na kurekebisha michoro na ramani inavyostahili kulingana na huduma zilizopo kwenye zabuni.
- Ionyeshe uwezo wa kufanya kazi ndani ya ratiba na bajeti ya Mradi.
- Uwezo wa usimamizi wa Afya Usalama na Mazingira uliothibitishwa kwa shughuli za ukarabati wa ofisi.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kazi data ya EWURA ya Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa konesha katika maombi haya.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani.
- Leseni ya biashara inayodhibitisha kufanya kazi hii.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11** alasiri saa za Afrika Mashariki (EAT), tarehe **21 Februari 2022 .** Kichwa cha Barua pepe kiwe **0010007463.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni) ya awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa taasisi za awali zenye vigezo baada ya taasisi hizo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

166939

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TAKUKURU isisubiri maelekezo ya viongozi

**RAIS** Samia Suluhu Hassan alimaliza ziara mkoani Mara juzi akiwa ameagiza wakaguzi wa ndani katika mkoa huo wabadilishwe vituo vya kazi kutokana na kuwapo na ufujaji wa fedha za miradi ya maendeleo zinazotolewa na serikali, hivyo kusababisha utekelezaji wa miradi mkoani humo kuchelewa.

Aidha, katika kuhitimisha ziara hiyo, mjini Bunda juzi, Rais pia aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Mara kuhakikisha inafuatilia kupambana ili kudhibiti matukio ya ufujaji wa fedha yanayoendelea ndani ya halmashauri.

Kwamba, ndani ya mkoa miradi kadhaa pesa zinafujwa, pesa zinaliwa na hakuna ripoti unayopita hadi mwaka ndio mkaguzi anasema, halmashauri haikufanya vizuri, kwamba madudu hayo hayaonekani kwa sababu wakaguzi wa ndani ni sehemu ya wafujaji wa fedha hizo.

Pia Rais Samia aliombwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kupeleka Sh. bilioni 24 kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere mjini Musoma hadi atakapojiridhisha kuwa zinakwenda kutekeleza kazi iliyopangwa, kutokana na kuwapo shaka ya matumizi yake.

Kutokana na maelekezo ya Rais, tunadhani kwamba ipo haja kwa TAKUKURU kuangalia uwezekano wa kuwa inachukua hatua mapema kuokoa fedha za Watanzania badala ya kusubiri malalamiko ya wananchi kwa viongozi. Tunaamini kwamba njia nzuri, ni watumishi wa taasisi hiyo kuwa na utaratibu wa kufuatilia miradi yote ya maendeleo mara tu inapoanza kutekelezwa, ili kujua hatua kwa hatua jinsi fedha za umma zinavyotumika.

Kwa njia hiyo na nyingine zinabuniwa na taasisi hiyo, inaweza kusaidia kuwabana wajanja wachache wanaojinufaisha kwa fedha za umma kutekeleza miradi chini ya kiwango na kuisababishia serikali hasara.

Rais anasema kazi ya taasisi hiyo ni kuzuia rushwa, na anaitaka ifanye kazi mara tu miradi inapoanza kwenye maeneo yao. Nasi tunaamini kwamba kwa utaratibu huo, fedha za umma zinaweza kuokolewa.

Watumishi wa taasisi kusubiri wananchi wapige kelele ndipo wafanye uchunguzi, tunaona kama watakuwa wamechelewa na watakuwa hawajapambana au hawajazuia rushwa kwa mujibu wa majukumu yao waliyopewa kisheria. Kwa maelekezo ya Rais, kuzuia vitendo vya rushwa, ndio kazi ya taasisi hiyo, siyo kusubiri ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ndipo ianze kufukuzana kwenda kuwadhibiti waliofanya makosa. Nasi tunamuunga mkono.

Tunaamini kwamba, TAKUKURU ina watumishi wenye taaluma mbalimbali ambao wanaweza kutumika katika vita dhidi ya rushwa na kusaidia kukomesha vitendo hivyo katika jamii ili kusaidia kuharakisha maendeleo.

Waswahili wana msemo kwamba; 'ukiona mwenzio ananyolewa, na wewe tia maji'. Hivyo tunadhani watumishi wa taasisi hiyo kote nchini watakuwa wamejifunza kutokana na maelekezo ya Rais kwa wenzao wa Mara.


Imani yetu katika hilo, inatokana na ukweli kwamba karibu maeneo yote nchini, mawaziri na viongozi wetu wakuu wa kitaifa akiwamo Rais katika ziara zao wamekuwa wakipokea malalamiko ya wananchi kuhusu kukwama kwa miradi ya maendeleo ingawa serikali inajitahidi kupeleka fedha.

Ni matarajio yetu kwamba, watumishi wa taasisi hiyo nchini watazingatia maelekezo hayo na kusimamia miradi yote ya maendeleo ikiwamo ya ujenzi wa barabara, shule, zahanati, maji na mingine mingi tangu inapoanza.

Hatua hiyo inaweza kusaidia watumishi wa TAKUKURU kubaini ubadhirifu wa fedha za umma na kuwachukulia hatua wahusika badala ya kusubiri kuletewa ripoti mezani ndipo wafuatilie.

Rushwa si tu adui wa haki, bali pia inachelewesha maendeleo, ndiyo maana tunashauri kuwapo na uvumbuzi na ubunifu wa kukabiliana nayo katika miradi ya maendeleo, kwa kufuatilia utekelezaji wake tangu mwanzo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# AU yahofia kasi kurejea wimbi la mapinduzi

**MAPINDUZI** ya serikali zilizochaguliwa na wananchi kupitia sanduku la kura, barani Afrika, yanaelekea kuwa kitisho kinachohofisha jumuiya ya kimataifa inapotizama hatima ya demokrasia kwenye mataifa hayo yanayojikongoja kimaendeleo.

Wiki iliyopita kwenye Mkutano wa 35 wa Umoja wa Afrika (AU) unaofanyika makao makuu ya umoja huo, Addis Ababa, viongozi wa nchi wanachama, wanajadili suala la ongezeko la mapinduzi ya kijeshi.

Mapinduzi hayo yaliyojitokeza kwa kipindi kifupi yanatikisa ukanda wa Afrika Magharibi na viongozi waliohudhuria mkutano huo, wanalilalamikia wimbi hilo.

Kikao hicho kinasema ni mara tano sasa kwa mwaka uliopita, serikali zimepinduliwa na kuandika historia.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, Februari 5, mwaka huu, akitoa hotuba kwa njia ya mtandao, kwenye mkutano huo, anasema AU ni chanzo cha matumaini duniani.

Anasema, ushirikiano kati ya UN na AU, una nguvu zaidi kuliko hapo awali, na kwamba ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu na ya 2063 ya Afrika Tunayoitamani-'The Africa We Watu', ni nguzo kuu.

Wakati Katibu Mkuu wa UN, anasema hayo, wakuu wa AU wanahitimisha mkutano kwa kulaani wimbi la mapinduzi, wakisema limesababisha mataifa kadhaa kusimamishwa uanachama katika umoja huo.

Rais wa Ghana, Nana Akufo-Addo, anasema mapinduzi yaliyotokea nchini Mali yameambukiza nchi nyingine akisema maofisa wa kijeshi wa mataifa jirani za Guinea na Burkina Faso.

Wakati mapinduzi ya Afrika Magharibi, yakijadiliwa mkutanoni, hatua ya jeshi kuchukua madaraka nchini Sudan, Oktoba mwaka jana, pia ilisababisha maandamano makubwa mitaani ya kudai kurejeshwa kwa utawala wa kiraia.

Ingawa inaelezwa, idadi ya mapinduzi barani Afrika, imekuwa ikipungua, kutokana na kuenea kwa uchaguzi na uhamishaji wa madaraka kwa njia ya amani, wimbi jipya linaanza kuleta hofu.

Nchi mbili ambazo jeshi limenyakua mamlaka hivi karibuni, Burkina Faso na Mali, zimekuwa zikijitahidi kuzuia uasi wa Kiislamu.

Aidha, wiki iliyopita, kulikuwa na jaribio la mapinduzi nchini Guinea-Bissau, ambalo Umaro Mokhtar Embaló aliyalaumu magenge ya ulanguzi wa dawa za kulevya.

Nchi hiyo iko kwenye sehemu kuu ya usafiri kati ya nchi zinazozalisha dawa za kulevya katika Amerika ya Kusini na masoko ya Ulaya.

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki Mahamat, anasema hali ilivyo inaleta hisia kuwa Afrika inarejea katika kipindi ambacho mapinduzi yalikuwa mambo ya kawaida, akisema ni jambo lisilokubalika.

Umoja wa Afrika, pia umelalamikiwa kwa kuchukua hatua zisizo sawa katika baadhi ya matukio, likiwamo la kutoisimamisha Chad, baada ya baraza la kijeshi kuongoza serikali, baada ya kifo cha kiongozi wa muda mrefu wa taifa hilo, Idriss Deby Itno, kilichotokea katika uwanja wa mapambano.

Tofauti na hayo, mjini Addis Ababa, Rais Uhuru Kenyatta amepongeza juhudi zilizofanywa na Afrika katika vita dhidi ya ugonjwa wa malaria, miaka miwili iliyopita.

Uhuru, alikuwa akiwasilisha ripoti ya hatua zililizopigwa katika makabiliano ya ugonjwa huo.

Umoja wa Afrika ni muungano wa mataifa 54 ya Afrika yenye lengo la kuimarisha ushirikiano wa kisiasa na kiuchumi wa bara hilo.

Maamuzi muhimu ya AU yanafanywa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika ambao unawakutanisha wakuu wa mataifa na serikali za nchi wanachama unaofanyika mara mbili kwa mwaka.

AU pamoja Kamisheni ya Umoja wa Afrika makao makuu yake yako Addis Ababa nchini Ethiopia.

TANGAZO

DON BOSCO NETWORKS TANZANIA

## PROPOSED CONSTRUCTION OF SANITATION FACILITIES TO BE BUILT ON PLOT No. 1 BLOCK B AT DIDIA SHINYANGA MUNICIPALITY - TANZANIA

**Tender number: DBDDS/0001/2022-23**

# INVITATION FOR TENDERS

**Date: [09th February 2022]**

1. Executive Director of Don Bosco Networks Tanzania invites sealed tenders for the Proposed Construction of Sanitation Facilities to be built on Plot No. 1 Block B at Didia Shinyanga Municipality, Tanzania.

2. The Executive Director of Don Bosco Networks Tanzania now invites sealed Tenders from eligible National contractors registered or capable of being registered in **Class 6 and above in BUILDING WORKS** for carrying out **the Proposed construction of Sanitation Facilities to be built on Plot No. 1 Block No. 'B" at Didia Shinyanga Municipality, Tanzania.**

**The project consists of the following works: -**

- The finalization of the boys' Sanitation Facility Block
- Construction of the girl's Sanitation Block
- Associated Building Engineering Services installations that is, Electrical, Plumbing (and drainage)
- Estimated project budget (320,000,000 Tsh)

3. Tendering will be conducted through the Don Bosco Network Tanzania tendering procedures. The tender is open to all tenderers as defined in the Public Procurement Regulations, Government Notice No.446 of 2013.

4. Interested eligible Tenderers may obtain further information from and inspect the Tendering Documents at the office of the Executive Director of the Don Bosco Network Tanzania at Oysterbay, P.O. Box 32770, Dar es Salaam from 0900 hours and 1630hours on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays. Alternatively, tenderers can request tendering documents through **executivedirector@dbtz.org; alfred_projects@dbtz.org; cassian_projects@dbtz.org**

5. All Tenders must be accompanied by Tender security in an acceptable form in the amount equivalent to 2.5% of Tender price or an equivalent amount in a freely-convertible currency.

6. All Tenders in **ONE ORIGINAL HANDWRITTEN [ INKED] HARDCOPY and a softcopy of Bills of Quantities in a flash disk in Excel format [ and not in PDF],** correctly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address at Executive Director, Don Bosco Networks Tanzania, P.O. Box 32770, Dar es Salaam at or before 1500hours, Monday, 21st February 2022.

7. Late Tenders, a portion of Tenders, electronic Tenders, Tenders not received by the deadline shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**Fr. MELCHADES NSHABA LUKANYANGA**
**EXECUTIVE DIRECTOR**
**THE REGISTERED TRUSTEES OF THE SALESIANS OF DON BOSCO TANZANIA**

166970

# Ripoti: Ufisadi unapoteza mapato asilimia 5 taasisi za umma, binafsi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RIPOTI ya kimataifa ya mwaka 2021 iliyotolewa na Taasisi ya Taaluma ya Kudhibiti Ufisadi Duniani (ACFC) inasema asilimia tano ya mapato yanapotea kwa ufisadi kwenye taasisi zote za umma na binafsi.

Mbobezi wa masuala ya kubaini ubadhirifu na kudhibiti rushwa na ufisadi, Shakibu Mussa Nsekela, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo taasisi hizo ili kudhibiti hali hiyo.

Alisema katika utendaji kazi wao wamebaini kuwa ufisadi ulioshika kasi ni ule unaosikika au kujulikana na ufisadi mwingi haugunduliki.


Alifafanua kuwa unapotokea ufisadi taasisi hutumia gharama kubwa namna kwa kufanya uchunguzi ukaguzi na fedha zilizochukuliwa kuzirudisha inakuwa ni tatizo.

"Tumeona njia bora ya kudhibiti ufisadi ni kuzuia ufisadi usitoke na inapotokea tujenge taswira na wahusika ipo siku watagundulika kuwapo na nia ya kuwatafuta watu kuwafuatilia ili wagundulike kazi yetu kubwa tunawajengea uwezo taasisi za umma na binafsi juu ya dalili za ufisadi namna gani zinatokea na jinsi ya kudhibiti ufisadi," alisema. Kwa upande wake, Wakili wa Kujitegemea na Mhadhiri wa Sheria Mwandamizi, Dk. Clement Mashamba, alisema tatizo la ufisadi ni kubwa kwa kuwa watu wengi wanaamini ili kuwa tajiri lazima mtu afanye ufisadi.

"Watu wamekuwa wakivunja sheria na taratibu zilizowekwa lakini usimamizi ni mdogo hali inayopelekea ufisadi kuendelea kutokea kikubwa tuangalie upya sheria zetu ili ziweze kubana mianya ya ufisadi na mambo yanayoibuka mapya katika ufisadi kwani sasa ufisadi upo kwenye njia za kidigitali mitandao," alisema

Naye Meshaki Shashi, Kaimu Mkuu wa Idara ya Uchunguzi wa Ndani Benki ya Taifa ya Biashara (NB), alisema mafunzo hayo ni muhimu kwao kwa kuwa yanawaweka kupambana na ufisadi katika maeneo ya taasisi za umma na binafsi.

"Ufisadi ni tatizo kubwa sio kwenye benki tu sehemu zote, lakini kwenye benki yangu ipo kama taasisi na ndio maana tupo hapa katika kuhakikisha tunapeana uwezo kudhibiti uhalifu huu," alisema.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (wa pili kulia), akipokea kompyuta kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania PLC, Sitholizwe Mdlalose (katikati) na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya African Child Project, Catherine Kimambo, ikiwa ni sehemu ya uzinduzi wa mradi wa uunganishwaji wa shule kidigitali katika shule 50 za umma kwenye mikoa 10 nchini, katika hafla iliyofanyika shule ya sekondari Mawenzi, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. Kulia ni Mwakilishi wa Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Arnold Msuya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ahimiza wananchi kupata elimu ya kodi

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Kanali Michael Mntenjele, amewataka wafanyabiashara kujitokeza kwa wingi kwenye kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango inayofanyika wilayani humo ili watoe kero zao na kupata ufumbuzi.

Akizungumza na timu ya maofisa kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA) wanaofanya kampeni hiyo ya elimu kwa mlipakodi wakati walipowasili wilayani humo jana, Kanali Mntenjele alisema ni muhimu wafanyabiashara kujitokeza kwa wingi kupata elimu ya kodi ili waelewe faida za kodi wanazolipa ndani ya nchi yao.

"Nitoe wito kwa wafanyabiashara wetu wa Tarime kama walipakodi wajitokeze kwa wingi na wawapokee waelimishaji wa TRA ili waweze kuwasilikiliza kwa lengo la kupata elimu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa sababu kodi hizo ndizo zinazoisaidia serikali kupata fedha kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa jamii," alisema.

Mfanyabiashara wa nguo wa wilayani humo, Zuhura Ally, alisema amefurahishwa na utaratibu huo na amepata fursa ya kutoa kero zake ambazo zimefanyiwa kazi na maofisa hao wa TRA.

"Kwa kweli ni jambo zuri TRA kujua wafanyabiashara tunaendeleaje na leo wameweza kutatua baadhi ya kero zangu na nyingine wameniambia nifike ofisini ili niweze kutatuliwa zaidi matatizo yangu," alisifu Zuhura.

Mfanyabiashara wa mapambo ya magari wa wilayani humo, Soti Warioba, alisema maofisa wa TRA wamebadilika kwa kiasi kikubwa tofauti na kipindi cha nyuma.

Alifafanua kuwa walipokuwa wanazunguka kwenye maduka mbalimbali kutoa elimu, hakuna mfanyabiashara aliyeogopa wala kufunga duka.

Timu ya maofisa wanaofanya kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango mkoani Mara, iko wilayani Tarime ikiendelea kutoa elimu ya kodi na baada ya wilaya hiyo, itakwenda wilaya zingine za mkoa huo.

# Kampuni zafunzwa sera ya uzalishaji mbegu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) kimetoa mafunzo kwa kampuni za uzalishaji mbegu juu ya sera, sheria na taratibu mbalimbali za mbegu ili waweze kufanya shughuli zao sambamba na maelekeo ya serikali.

Lengo ni kuongeza uzalishaji wa mbegu bora hali itakayosaidia kuongeza tija ya mazao kwa wakulima nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungua mafunzo hayo yanayofanyika jijini Arusha, Meneja wa Sera kutoka SAGCOT, Khalid Mgalamo, alisema mafunzo hayo yamelenga katika kuwajengea uwelewa kampuni ya mbegu nchini juu ya sera na sheria za nchini na kutoa mapendekezo ya kuboresha sera hizo ili kufanya uzalishaji wa mbegu bora na kuboreshwa zaidi.

"Lengo kubwa ni kuwapitisha kwenye sera za mbegu na kujadili changamoto zinazoikabili sekta ya mbegu na kuja na mapendekezo ambayo yanafikishwa katika ngazi husika kwa maamuzi zaidi ili kuboresha mazingira ya uzalishaji mbegu nchini," alisema Mgalamo.

Alisema wazalishaji wa mbegu ni wadau muhimu katika kuendeleza kilimo kwa kuhakikisha mbegu bora zinapatikana kwa wingi kote nchini ili kukidhi mahitaji na kupelekea tija katika uzalishaji mazao yenye ubora kuongezeka na kuingia kwenye soko la ushindani. "Nchi itakapojitosheleza kwenye kuzalisha mbegu bora kupitia kampuni ya hapa nchini itawezesha kupunguza uagizaji wa mbegu kutoka nje ya nchi kwa fedha za kigeni," alisema Mgalamo.

Alisema SAGCOT itaendelea kuratibu mafunzo na vikao mbalimbali kwa wadau wake na taasisi za serikali kwa lengo la kujadili changamoto na kuja na mapendekezo yatakayosaidia kuboresha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi nchini.

"Mbegu ndiyo kiungo katika kilimo, bila mbegu hakuna kilimo, hivyo kuna kila sababu ya kushirikiana pamoja kama wadau wa sekta hii kuhakikisha mazingira ya uzalishaji kwa kampuni za ndani yameboreshwa ili wazalishe mbegu kwa tija," alisema.

Mgalamo aliongeza kuwa kampuni za mbegu ni sehemu ya kuzalisha ajira kwa vijana nchini sambamba na kuongeza tija ya uzalishaji katika sekta ya kilimo.

Mkurugenzi Mtendaji Tanzania Seeds Traders Association (TASTA), Baldwin Shuma, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwani yanazidi kuboresha sekta zaidi tunaiomba serikali kuhakikisha wanatenga maeneo katika halmashauri ili kampuni za mbegu ziweze kupata aridhi wafanye uzalishaji wao ambao utakuwa na tija kwa kuhakikisha mbegu bora zinapatikana kwa wingi nchini na kupunguza uagizaji wa mbegu kutoka nje ya nchi.

"Tunaiomba Serikali katika halmashauri zetu kutenga maeneo kwa ajili ya kampuni ya mbegu kufanya uzalishaji wa mbegu kuwa na uhakika wa aridhi ya kufanyia uzalishaji wa mbegu jambo litakalomjengea mwekezaji uhakika wa biashara yake," alisema Shuma.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Majaribio ya Kitaifa ya Umahiri wa Mbegu kutoka TOSCI, Dk. Adolf Saria, alisema SAGCOT inafanya kazi nzuri katika kuunganisha wadau katika kujadili changamoto mbalimbali katika sekta ya kilimo kupitia vikao kama hivi ambapo mapendekezo yatakayopatikana yatakwenda kusaidia katika kuboresha sekta.

"TOSCI ipo katika kutoa ithibati ya mbegu hivyo itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo kuhakikisha mbegu zinazozalishwa zinakidhi viwango vya ubora ili kuongeza uzalishaji wa mazao," alisema Dk. Saria.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bytrade (T) LTD, Harish Dhutia, ameishukuru SAGCOT kwa kumwalika katika mafunzo hayo na kusema mafunzo kama hayo yanaonyesha dhamira ya kweli katika kuboresha sekta ya kilimo nchini.

# Wanaotumia jina la TRA kutapeli watangaziwa vita

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) mkoa maalumu wa kikodi Kahama, imetangaza vita kwa baadhi ya wananchi ambao sio waadilifu wanaojifanya maofisa wa mamlaka hiyo na kujipitisha kwa wafanyabiashara na kuwakagua kisha kujipatia fedha kinyume cha sheria.

Kadhalika, imewaonya baadhi ya wafanyabiashara ambao wamekuwa wakichukua risiti za mashine za EFD katika vituo vya mafuta na kuambatanisha wakati wa upigaji wa hesabu za kila mwaka kwa madai walitumia wakati wa usafirishaji wa mzigo wa mteja wakati si kweli.

Meneja wa Ukaguzi wa Mamlaka hiyo, Irene Hans, alitoa angalizo hilo alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari ofisini wake juu ya kampeni ya 'Kamata Wote' inayokwenda sambamba na utoaji wa elimu kwa wafanyabiashara na wanunuzi kuhusu kutoa na kudai risiti ya EFD mashine baada ya manunuzi ya biashara yoyote.

Alisema wamekuwa wakifanyakazi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, hivyo watakapoanza zoezi la kuwabaini watu wanajipitisha kwa wafanyabiashara na kujifanya wakaguzi wa kodi watahakikisha wanawajibishwa kisheria, kwa sababu wamekuwa wakichafua mamkala kwa vitendo hivyo.

Pia Hans aliwatadharisha wafanyabiashara ambao wamekuwa wakitoa risiti za EFD zenye kiwango ambazo haziendani na thamani ya mzingo ulionunuliwa, waache mara moja kwa sababu huo ni wizi kama ulivyo wizi mwingine kabla hawajaanza kuchukuliwa hatua.

"Kuna baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakitoa risiti za EFD kwa wateja wao ambazo haziendani na thamani ya mzigo wao, mzingo wa shilingi 100,000 wanatoa risiti ya shilingi 10,000... jambo hili bado tunaendelea kulikemea na wahusika watakapobainika adhabu kali zitachukuliwa," alisema Hans.

Aliongeza: "Kwa mfanyabiashara atakayebainika kutotoa risiti kwa mteja wake faini yake itakuwa Sh. 3,000,000 mpaka milioni tano huku kwa mteja ambaye hatadai risiti hiyo pia atatozwa faini ya Sh. 300,000 mpaka Sh. milioni 1.5, hivyo kila mmoja kudai na kutoa risiti kwa kila bidhaa inayotoka na kuingia.

Mmoja wa wafanyabiashara wa mjini hapa, Godfrey Masumbuko, alisema miongoni mwa wanaoichafua mamlaka hiyo ni wanaowasumbua wafanyabiashara kwa kujiita maofisa wa TRA ambao wanapita na kufanya ukaguzi wa utoaji wa risiti kumbe wanataka fedha.

Alisema, mwaka juzi kulikuwa na kijana mmoja aliyejifanya mtumishi wa TRA na alikuwa akivaa kama watumishi, lakini baada ya kufuatilia na kutambua sio mhusika, aliwajibishwa kisheria na alikuwa akitapeli wafanyabiashara wa Mji Mdogo wa Kagongwa.

Naye Lucy Mayengo alisema, kila biashara ambayo amekuwa akiifanya na wateja wake anahakikisha anatoa risiti na kuwapatia kwa sababu inamrahisishia katika utunzaji wa kumbukumbu za mauzo na ukadiriaji wa mapato kila mwaka na imesaidia kuondokana na msuguano na maofisa wa TRA.




Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Amani, Kata ya Kipunguni, jijini Dar es Salaam, Daniel Malagashimba (kushoto), akikabidhi msaada wa moja ya maboksi manne ya madaftari kwa Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kata ya Kitunda, Fatuma Abdulrahman, kwa ajili ya wanafunzi wa mtaa huo, juzi. Wengine ni viongozi wa kituo hicho. **PICHA: SABATO KASIKA**

# H/shauri yaja na mkakati kuboresha usafi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

HALMASHAURI ya Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi imeanza kutoa tuzo ya cheti kwa kata zinazofanya vizuri kwenye suala la usafi.

Akizungumza katika kikao cha watendaji wa kata, mitaa na madiwani, Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Mpanda, Sophia Kumbuli, ameitaja Kata ya Kashaulili kuongoza katika usafi na kuizawadia cheti cha usafi kwa mwezi Januari 2022 pamoja na fedha taslimu shilingi 100,000.

Katika hatua nyingine kwenye zoezi la kuzitambua kata zinazofanya vizuri katika suala la usafi, Kata ya Shanwe imeshika nafasi ya pili huku Kata ya Majengo ikishika nafasi ya tatu kwa usafi.

Kata ya Kawajense imetajwa kuwa ya mwisho kwa usafi na kuzawadiwa kinyago cha uchafu ikiwa ni ishara ya kuhakikisha kata hiyo inajipanga vizuri katika usafi wa mazingira.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Kashaulili, Magreth Kitungulu, amesema wao wamejiwekea utaratibu wa kila Alhamisi kuhamasisha wakazi wa kata hiyo kufanya usafi katika maeneo yao ili kuimarisha na kuendeleza usafi.

Naye Diwani wa Kata ya Kawajense, Uwezo Bachu, aliupongeza mpango wa usafi katika Manispaa ya Mpanda, na wao Kata ya Kawajense wamepokea kinyago hicho kama changamoto ya kuwafanya viongozi wa kata kuongeza bidii katika usafi na kuahidi kufanya vyema kwa kipindi kijacho.

Meya wa Manispaa ya Mpanda, Haidary Sumry, alisema Baraza la Madiwani katika vikao vyao ajenda ya usafi wa Manispaa ya Mpanda imekuwa ya kudumu kwa kuhamasisha madiwani kuendelea kusimamia usafi kwenye kata zao, hivyo zoezi hilo litatia chachu ya kufanya usafi kwa kiwango kikubwa katika Manispaa ya Mpanda.

## Wakala kusambaza tani 2,000 za alizeti

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKALA wa Mbegu za Kilimo (ASA) umesema umejipanga kupeleka tani 2,000 za mbegu za alizeti kwa wakulima ili kukabiliana na uhaba.

Mtendaji Mkuu wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, alisema tani 1,650 wameshazisambaza kwenye vituo vyao mbalimbali vya mauzo.

Dk. Kashenge alisema mbegu walizosambaza ni za kilimo cha muda mfupi zinazoendana na changamoto ya jua na joto iliyoikumba nchi katika mwaka 2021 na kusababisha uhaba wa mvua.

Aliwashauri wakulima kuzitumia mbegu hizo za muda mfupi na za kustahimili ukame ambazo pia zinatumia uchavushaji huria.

Aidha, Dk. Kashenge alisema ASA imefanikiwa kuongeza uzalishaji wa mbegu mbalimbali kutoka tani 1,749 mwaka 2019/20 hadi tani 3,333 mwaka 2020/21 kutoka kwenye mashamba yake 14.

## Atakayemwona Mzee Mbalamwezi atoe taarifa

**Na Christina Mwakangale**

MKAZI wa Kimara Baruti mkoani Dar es Salaam, Beatus Mbalamwezi (76), anatafutwa na familia yake baada ya kutoweka nyumbani kwa binti yake eneo la Kifuru, Kinyerezi, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe, Anna Mbalamwezi, alisema, baba yao akiwa na mkewe, alikwenda kumsalimu binti yao mwingine aishiye Kifuru, lakini baada ya muda mfupi walipomuacha sebuleni na waliporejea hawakumkuta.


Alisema baada ya tukio hilo walifika eneo la kituo cha daladala Segerea na Kisukulu na kwamba wenyeji wa eneo hilo walidai kumuona na akipanda daladala.

"Mzee anasumbuliwa na tatizo la kusahau, mara ya mwisho alionekana Kifuru, Sabato juzi, saa 10 jioni, alikuwa amevaa kofia nyeusi, shati la mikono mirefu jeusi lina maua meupe, suruali ya kaki na viatu vyeusi vya kamba, pia ni mrefu.

"Tunaomba sana atakayemwona tuwasiliane kwa namba 0719 233577, 0716 031626 au 0654 175696. Tumetoa taarifa kituo cha polisi Stakishari na kupewa faili namba STK/RB/1395/2022," alisema Anna.

Pia alisema jana walifika eneo la Segerea, Gongo la Mboto, huku wenyeji wa eneo hilo wakidai aliingia kwenye moja ya duka la dawa Kisukulu, ila hawakujua ameenda wapi.

"Siku ya pili tumerudi Segerea kuulizia baadhi ya watu wakadai alionekana muda fulani, ila hatujampata kwa sasa tumeacha taarifa akionekana watupigie."



# Vitongoji 37,610 havina umeme

BUNGE limeelezwa kuwa serikali imefanya uhakiki na kuainisha uwapo wa vitongoji takribani 37,610 visivyokuwa na umeme Tanzania Bara.

Aidha, inakadiriwa Sh. trilioni saba zitahitajika ili kukamilisha mahitaji ya umeme katika vitongoji hivyo.

Wizara ya Nishati ilitoa majibu hayo jana bungeni katika swali la Mbunge wa Mbarali (CCM), Fransis Mtega.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itakamilisha kuvipatia umeme wa REA vitongoji na vijiji vilivyobaki katika Jimbo la Mbarali.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema serikali imeanza utekelezaji wa miradi ya ujazilizi unaolenga kufikisha umeme katika vitongoji vyote Tanzania Bara awamu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ikiwa ni pamoja na vitongoji vya Jimbo la Mbarali.

Aidha, ilisema kati ya vijiji 102 vya Wilaya ya Mbarali, vijiji 20 bado havijapatiwa umeme.

Ilisema vijiji hivyo 20 vinapatiwa umeme kupitia mradi wa REA III mzunguko wa pili ambao unaendelea kutekelezwa na mkandarasi ambaye ni M/S Electrical Transmission and Distribution Construction and Maintenance Co. LTD.

Ilibainisha kuwa mkandarasi amekamilisha kazi ya usanifu wa kina, upimaji, uandaaji wa michoro na anaendelea na manunuzi ya vifaa pamoja na kusimika nguzo katika maeneo ya mradi.

Ilisema gharama ya mradi ni Sh. bilioni saba na utekelezaji unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022.




Habari zote na Augusta Njoji



Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria na Katiba, Najma Murtaza Giga, akiwasilisha maoni ya kamati hiyo, kuhusu muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali namba 7 ya mwaka 2021, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# ATCL yaagizwa kufanya utafiti nauli za mashirika washindani

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), ameagizwa kufanya utafiti wa nauli zinazotozwa na mashirika ya ndege washindani kwa safari za ndani, ili kuziwianisha na kupanga nauli zinazovutia Watanzania wengi kutumia ndege za ATCL.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilitoa agizo hilo jana bungeni ilipokuwa ikitoa majibu ya swali la Mbunge wa Gando (CCM), Mussa Omar Salim.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji sababu za mabadiliko makubwa ya bei za tiketi za ndege za ATCL zinazofanya safari zake Dar es Salaam na Dodoma na kudai kuwa mara nyingi hufika hadi Sh. 600,000.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema mfumo wa uuzaji wa tiketi katika biashara ya usafiri wa anga ni mojawapo ya mikakati ya ushindani ili kuvutia wateja.

Ilifafanua kuwa mashirika ya ndege hushindana kwa kutumia mkakati huo ambapo tiketi hupangwa katika ngazi mbalimbali kufuatana na vigezo mbalimbali kama vile bei ya tiketi, ujazo wa ndege, muda wa kukata tiketi, masharti ya tiketi na daraja la usafiri.

Hata hivyo, ilisema kwa kutumia kigezo cha ujazo wa ndege na muda ambao abiria anakata tiketi, mteja anayekata tiketi mapema na kukuta ndege haijajaa hupata bei za chini ukilinganisha na mteja anayekata tiketi muda mfupi kabla ya safari yake na kukuta ndege imejaa, ambapo mara nyingi huwa siku chache au muda mfupi kabla ya safari, hupata bei za juu.

Ilisema mfumo huo unatumika kimataifa na mashirika yote ya ndege na kwa ATCL bei hizo zimepangwa katika ngazi mbalimbali kwa mfano katika safari ya Dodoma kwenda na kurudi.

Ilieleza kuwa ATCL ina jumla ya ngazi 13 katika daraja la kawaida ambapo bei zake zinaanzia Sh. 331,400 hadi Sh. 678,400.

Pia ilisema bei ya juu ya wastani wa Sh.600,000 ni viti 10 kati ya jumla ya viti 76 vya ndege nzima sawa na takribani asilimia 13 ya ujazo wa ndege.

Vilevile, ilisema kuna daraja la ambalo kuna viti sita tu na ni kwa abiria yoyote ambaye yupo tayari kulipa katika daraja hilo.

Ilibainisha daraja hilo linatoa huduma maalum kwa mfano mteja anapewa kilo saba zaidi za mizigo ukilinganisha na daraja la kawaida, mteja hupatiwa mhudumu wa kumsikiliza kwa haraka muda wowote akiwa ndani ya ndege.

Kutokana na sababu hizo, ilisema gharama za daraja hilo ni kubwa kuliko daraja la kawaida ambapo daraja hilo lina ngazi nne zenye bei kati ya Sh. 721,600 hadi Sh. 953,000.

## Mbunge aomba gari la zimamoto Uwanja wa Ndege Mtwara

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, amesema Uwanja wa Ndege wa Mtwara unakabiliwa na tatizo la ukosefu wa gari la zimamoto na kuiomba serikali kukamilisha mchakato wa manunuzi ya gari hilo.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Chikota alisema fedha ya kununua gari hilo ipo kwenye hatua ya kwanza ya ukarabati wa uwanja na kutaka kujua serikali itakamilisha lini ununuzi wa gari hilo.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa akijibu swali hilo, alikiri kuwapo ukosefu huo na kwamba mchakato wa ununuzi wa gari hilo unaendelea na kiasi cha Sh. bilioni 1.5 kimetengwa.

Pia alisema tayari mkandarasi amepatikana wa kupeleka gari hilo.

Awali, Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Anastazia Wambura, alihoji lini serikali itajenga mnara wa kuongozea ndege wenye urefu wa kutosha kumwezesha mwongoza ndege kuona miundombinu yote ya njia ya ndege kwenye uwanja huo.

"Je, ni lini serikali itajenga jengo la muda la abiria lenye ukubwa wa kutosha wingi wa abiria wanaoingia na kutoka katika uwanja huo? Je, ni lini 'parking shade' ya mitambo ya zimamoto na uokoaji itajengwa katika eneo lililopangwa kwenye 'master plan'?"Alihoji.

Prof. Mbarawa akijibu maswali hayo, alisema kiwanja hicho kilijengwa na kuanza kutoa huduma katika miaka ya 1952/53 na kutokana na kuongezeka kwa matumizi yake yanayotokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii katika mikoa ya kusini kilihitaji kufanyiwa maboresho makubwa.

"Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), iliandaa mpango kabambe (master plan) uliopendekeza kupanua kiwanja hiki kutoka daraja Code 3C kwenda Code 4E (kwa mujibu wa ICAO). Kiwanja kitakapokamilika, kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa za ndani na nje ya nchi zenye ukubwa wa Boeing 787-8 (Dreamliner),"alisema.


Aidha, alisema uboreshaji wa kiwanja hiki umegawanywa katika awamu mbili, ambapo kwa sasa ujenzi unaoendelea ni wa awamu ya kwanza unaohusisha baadhi ya kazi zikiwamo urefushaji wa njia ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa maegesho mapya ya ndege na barabara zake za maingilio.

"Naomba nimhakikishie mheshimiwa mbunge kuwa ujenzi wa mnara wa kuongozea ndege, jengo la abiria na kivuli kwa ajili ya maegesho ya mitambo ya zimamoto, vitajengwa katika awamu ya pili baada ya awamu ya kwanza kukamilika," alisema.

KUELEKEA UCHAGUZI KENYA...

## Raila aendelea kubaki 'mtoto wa Baba' - Rais Kenyatta

Ukurasa 13





Ukurasa 14



**WAZIRI MKUU BORISS JOHNSON UINGEREZA WAAMSHA 'DUDE', KISA MISURURU YA TAFRIJA 'HARAMU'**



MIAKA 45 CCM

# Chama kinakwenda na wakati, lakini kinabanwa

•Ni hofu kuogopa nguvu ya soko, ubinafsishaji

**Na Ani Jozeni**

KUTAFAKARI njia iliyofuatwa au inayofuatwa na Chama Cha Mapinduzi miaka 45 baada ya chama hicho kuundwa Februari 5, 1977 ni jambo lenye mapana na marefu tofauti, kulingana na kila anayefanya uchambuzi huo.

Kwanza kuna upeo wa kukiangalia chama, kwani kila mmoja anakuwa na hisia chanya zaidi kuhusu kipindi alichoifahamu CCM, halafu alinganishe na yaliyotokea baadaye, inamaanisha kuwa vizazi tofauti vina sura tofauti za chama, na hisia mbalimbali au uthabiti, maadili ya uongozi katika kipindi kilichopita hivyo, hakuna njia ya 'kusawazisha' taswira hizo.

Wakati chama kinaadhimisha miaka 45, kitakachoangaliwa siyo yaliyopita au kulitokea nini ila makada, wanachama na jamii kwa jumla inavyojipanga katika utii na hamasa ya sera zinazofuatwa na uongozi wa wakati huu. Ndiyo hapo kimsingi kuna tofauti, kuwa hadi mwisho wa awamu ya tano kulikuwa na 'kwenda sawa' kati ya upeo wa wanachama na upeo wa uongozi, ila awamu ya sita imeleta kitu tofauti. Wanachama hawahitaji tu kuona kinachotokea na kutazamiwa kuunga mkono, ila sasa kuna suala la kuelewa nini mwelekeo, usahihi wake ni upi.

Kila awamu kimsingi imekuwa na changamoto yake kufikia mwelekeo mpya wa uongozi na upeo wa wanachama na jamii kwa ujumla, kuhusu nini kinafaa na nini kinawezekana. Kwa maana hiyo awamu tofauti zimekuwa na michango ya kipekee, kwa mema au mabaya kuhusu nini kinawezekana, kwa msingi wa kuhuisha na kupatanisha iwe migongano au matazamio katika jamii kwa jumla. Hulka ya kiongozi aliyepo na atakayotanguliza yana umuhimu, pia ndiyo msingi wa kujenga mwelekeo mpya, au mwendelezo wa mwelekeo wa jumla alioukuta.

Angalizo lililopo ni kuwa takriban kila awamu imefaulu pale ilipochukua hatua wakati wa kuingia madarakani kutatua changamoto ndani ya mwelekeo uliopo na ilipoanza hatua za kujenga mwelekeo mpya katika fani moja au nyingine ya uongozi.



Naibu Katibu Mkuu CCM –Bara, Christina Mndeme, mwanamama wa kwanza kushika wadhifa huo. CCM ikibadilika na kwenda na wakati. **PICHA: MTANDAO.**

Awamu ya kwanza ilipendwa bila minong'ono kati ya mwaka 1962 na 1967 wakati wa Azimio la Arusha, lililotokana na chama cha Tanu chini ya Mwalimu Julius Nyerere, Baba wa Taifa, kuhitaji ukaribu maalumu .

Aidha, wanafunzi wa Chuo Kikuu (kishiriki) cha Dar es Salaam kuandamana Oktoba 1966 kupinga kujiunga kwenda Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa miezi sita na kukatwa mshahara ili kusaidia maendeleo kwa miezi 18,ilitoa ishara zao kisiasa na kama jamii kwa ujumla.

Pamoja na kuwa Azimio la Arusha lilijenga mwelekeo wa kudumu wa kiitikadi miongoni mwa wasomi na ngazi za juu za watumishi serikalini na mashirika ya umma, sababu zao zilitofautiana. Wakereketwa ndani ya TANU walipenda Ujamaa kama itikadi, hali kadhalika watumishi serikalini walikuwa na lao la ziada wakiona Ujamaa kama mwendelezo wa 'Uafrika na Uzawa' wenyewe wasomi wakiuita 'Africanisation' ukiwa mkakati wa kuwaondoa Wazungu serikalini.

Azimio likafungua hatua ya kuwandoa wageni katika mashamba makubwa waliyokuwa wanamiliki, halafu na njia kuu za uchumi, kwa maana ya kununua na kuuza nje, mabenki, bima, umeme na uendeshaji bandari, serikalini waliona shughuli hizo sasa zitasimamiwa na wazawa.

Tafsiri hiyo ya Ujamaa na Kujitegemea isiyo rasmi na inayoeleweka kisaikolojia kwa wengi,inaendelea kuwa kati ya ishara chanya,hasa katika kukubaliana hata ikabaki katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuwa Tanzania ni nchi inayofuata siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Itakumbukwa kuna wakati Miiko ya Uongozi (kutoshiriki shughuli yoyote ya kibepari, yaani kutafuta fedha kibiashara, nje ya mshahara, kwa uwekezaji na kuwaajiri wengine) iliondolewa mwaka 1991 kwa 'Azimio la Zanzibar,' au Tangazo la Zanzibar.

Inawezekana wapo baadhi ndani ya jamii wawe wanasiasa au wengineo kuna yanayowachanganya ndani ya mageuzi hayo. Kwa mfano dhana 'kukopa na kuwa na deni kubwa la taifa kutasababisha nchi kupigwa mnada.'

Tatizo la kuogopa nguvu ya soko na masuala ya ubinafsishaji pamoja na uwekezaji wa kigeni ni mtihani ambao siyo rahisi sana, hata hivyo uchumi kitaifa unaenda mbele pale kunakuwapo mazingira huru, hakuna ubaguzi wa nani ana uwezo wa kuuza au kununua.

Unapotokea mkanganyiko wa kimilki au kibiashara kuainisha jamii, mathalan kitu fulani ama wasimilikishwe au kuuziwa Wazungu, Wahindi, au Waarabu ni dhana inayokwamisha nyendo za kiuchumi.

Mifumo ya kihistoria kama ufugaji wa ng'ombe wengi au maeneo ya kikabila ambako ardhi haina mwenyewe, ila ni ya ukoo yanaweza kuzuia mitaji kutoka nje, kupanuka soko na kuajiri vijana na wasomi kwa jumla katika rasilimali tarajiwa.

Hiyo ikitimizwa katika namna sahihi itaendeleza jadi iliyopo kwenye CCM hivi sasa kufanua ulazima wa uhuru wa kiuchumi katika mazingira huru, lakini yanayotoa kipaumbele kwa maendeleo ya Watanzania kupiga hatua kila kukicha.



Stephen Wasira, mwanasiasa anayetaka kuzingatiwa msimamo wa chama kumpata kiongozi wa taifa. **PICHA: MTANDAO.**

# Wachambuzi: Wasira yuko sawa kuzungumzia urais

## *Hajampigia debe Rais, anasimamia misingi ya chama

**Na Sabato Kasika**

SIKU moja baada ya mwanasiasa mkongwe wa CCM, Stephen Wasira, kutaka Rais Samia Suluhu Hassan, aachwe amalizie vipindi viwili vya urais, kama ulivyo utaratibu wa chama hicho, baadhi ya wachambuzi wa siasa wanatazama maoni yake, wakisema anachosema ni msimamo wa chama na si kuanzisha kampeni.

Miongoni mwa wachambuzi hao ni Abbas Mwalimu ambaye anasema, mkongwe huyo wa siasa hamkumpigia debe Rais Samia bali anataka yale ambayo chama kimejiwekea katika kumpata mkuu wa nchi yazingatiwe.

Anaeleza kuwa Wasira anazungumza kwa nia nzuri ambayo inalenga kuimarisha umoja ambao unaweza kukisaidia chama kuendelea kuwa madarakani, kwa kutaka wana CCM kuzingatia utaratibu ambao chama kimejiwekea katika kumpata mkuu wa nchi.

Anasema, kuna changamoto zilijitokeza mara baada ya Rais kuingia madarakani na akaziweka wazi kwamba wapo watu wanajipanga kwa ajili ya mwaka 2025 na kuwataka waache mtindo huo wachape kazi.

“Wito huo wa Rais unatokana na kwamba, kuwazia urais kunaweza kusababisha wasaidizi wake kushindwa kuwatumikia wananchi, hivyo hata Wasira alilenga kile ambacho kinahimizwa na Rais mwenyewe,” anasema.

Anasema, msisitizo wa Wasira uko hapo, kuwa CCM kuna utaratibu wake, na kwamba yeye ni mzee wa chama, anajua kuwa watu wakikaa na kuwaza urais, wanaweza wakashindwa kuwatumikia wananchi.

> “Wito huo wa Rais unatokana na kwamba, kuwazia urais kunaweza kusababisha wasaidizi wake kushindwa kuwatumikia wananchi, hivyo hata Wasira alilenga kile ambacho kinahimizwa na Rais mwenyewe,” anasema.

Mchambuzi huyo anasema hali hiyo isipodhibitiwa, watashindwa kutumikia wananchi, na watamwangusha Rais na hata wao wenyewe katika maeneo yao kwa kutoleta maendeleo na kuwafanya wapinzani kuwa na hoja.

### WASIRA YUKO SAHIHI

Godwin Gonde ni mchambuzi wa siasa na Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia Dar es Salaam ambaye anasema, Wasira yuko sahihi na kwamba wakongwe wa CCM wajitokeze kama yeye kukemea mbio hizo za urais, wakati huu ambao ndiyo kwanza serikali ya awamu ya sita inashika usukani.

“Kuelekea mwaka 2025, kumekuwapo na harakati ndani na nje ya CCM za kutaka urais, hali inayoweza kusababisha shughuli za maendeleo zikakwama. Wakongwe wa CCM waendelee kukemea,” anasema Gonde.

Anasema, Wasira amejitokeza hadharani kuwataka makada wenzake kufuata misingi na taratibu za chama zilizowekwa kwa ajili ya kumpata mgombea urais, na kwamba wengine zaidi wajitokeze kumuunga mkono.

“Wakiamuachia Rais pekee yake akemee, zinaweza kuibuka kambi ambazo zitaendelea kusaka nafasi hiyo na kuweka pembeni misingi ya chama, hali ambayo inaweza kuifanya CCM ikose umaarufu mbele ya jamii,” anasema.

Gonde anasema, mwaka 2025 bado uko mbali, na kwamba kinachotakiwa ni kuhimiza shughuli za maendeleo kama ambavyo Rais amekuwa akielekeza badala ya kuwaza urais wakati huu.

### RAIS SAMIA AACHWE

Katika mkutano wa hadhara mjini Bunda mkoani Mara juzi, mkongwe wa siasa nchini, Stephen Wasira, ambaye aliwahi kuihama CCM na kujiunga na NCCR-Mageuzi, anakumbusha kuwa Rais Samia aachwe amalizie vipindi viwili vya urais kama ilivyo utamaduni wa Chama Cha Mapinduzi.

Wasira ambaye amekuwa kwenye uongozi tangu awamu ya Baba wa Taifa ameshika nyadhifa mbalimbali serikalini kama ukuu wa mkoa, uwaziri akiongoza wizara kadhaa ikiwamo kilimo, aidha amekuwa mbunge wa Bunda Mjini kwa miongo mingi na katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 aliondolewa kwenye nafasi hiyo na Esther Bulaya wa CHADEMA.

Akiwa katika mkutano huo wa Rais Samia, aliyekuwa anahitimisha ziara ya siku mbili mkoani Mara, Wasira alipewa nafasi ya kuzungumza baada ya Rais kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa chujio la maji mjini Bunda.

Rais alikwenda kwenye maadhimisho ya jubilii ya miaka 45 ya CCM iliyofanyika mkoani Mara Jumamosi Februari 5. Akitoa kauli hiyo, Wasira anasema:.

“Wale waliosema wanataka urais 2025, mimi nawashauri wasubiri kwa sababu kwa utamaduni wa CCM kama kuna aliyepo ofisini huwa hatumpingi, tunampa nafasi amalizie awamu hiyo ambayo ni miaka 10.”

Anatoa mfano wake binafsi kwamba, aliwania urais mwaka 2015, lakini hakuupata na sasa kwa kuwa ameshapitwa na umri wa kugombea, amekaa pembeni na hana nia tena wala mpango wa kuwania nafasi hiyo.

Wasira anawataka wenye dhamira hiyo ya urais wasubiri hadi vipindi viwili vya Rais Samia vipite, na iwapo watakuwa wamepitwa na umri kama yeye waige mfano wake, ambaye amejiunga na wazee wa Mara, kwa kuwa si wote lazima kuwa rais bali ni fursa ya mtu mmoja.

Habari za kugombea uongozi wa urais 2025 si ngeni majukwaani kwani Rais Samia aliwahi kuwaeleza wanawake kuwa Rais mwanamke, watamweka 2025, na kuwashauri kufanya siasa vizuri kwa kukishikamana ili kumweka rais wao akiwahakikishia kuwa atasimama kwenye uongozi wa urais wakati ukifika.

KUELEKEA UCHAGUZI KENYA...

# Raila aendelea kubaki 'mtoto wa Baba' - Rais Kenyatta

## Martha Karua, Gideon Moi, Kalonzo rasmi kwa Ruto

**Na Christina Mwakangale**

IMEBAKIA miezi sita kufikia uchaguzi mkuu wa Kenya, unaotarajiwa kufanyika Agosti 9, huku joto la kisiasa likipanda wakati wote kutokana na kila mtia nia kujinadi ama kunadiwa na viongozi maarufu nchini humo.

Uchaguzi huo wa Rais utakwenda sambamba na kuwapigia kura wabunge pamoja na maseneta kwa mujibu wa katiba ya nchi hiyo na sheria za uchaguzi zilizofikiwa baada ya kuandikwa katiba mpya .

Utawala wa Rais Uhuru Kenyatta ulioingia madarakani tangu 2013 kupitia chama cha Jubilee, unatarajia kupisha kiti hicho kwa awamu nyingine baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Joto ni kali zaidi hasa kwa wanaowania urais wakiwamo viongozi waliomo na waliowahi kushika nyadhifa serikalini, akiwamo Naibu Rais William Ruto na Waziri Mkuu mstaaafu, Raila Odinga, ambaye kwa sasa anaungwa mkono na yuko karibu na Kenyatta.

Kwa Kenya huu ni uchaguzi wa 12 tangu ule wa kwanza mwaka 1969 ukifuatiwa uchaguzi zingine miaka ya 1974, 1978, 1979, 1983, 1988, 1992, 1997, 2002, 2007, 2013 na mwaka 2017 kwa mujibu wa mtandao wa taarifa za uchaguzi za Kenya .


Mwaka 2013, hofu ilitawala kutokana na ghasia za mwaka 2007 hadi 2008 na kusababisha kuzuiliwa kwa uchaguzi. William Ruto ambaye anatarajiwa kuwania wadhifa huo, amejipanga na chama chake ambacho si kilichomuingiza madarakani cha Jubilee, bali kipya cha United Democratic Alliance (UDA).

Sera za UDA ni kujali maslahi ya Wakenya wa tabaka la chini, wanaohangaika kila siku kusaka tonge ili angalau wapate mlo, hayo ni ya Ruto wakati Odinga naye, ameunda vuguvugu jipya la kisiasa linalofahamika kama Azimio la Umoja huku akipata uungwaji mkono na Rais Kenyatta.

Ahadi za Naibu Rais ni kwamba, atabadilisha uchumi wa wananchi wa hali ya chini iwapo ataingia madarakani.

Hii ni mara ya kwanza kwa Ruto ambaye kutofautiana kisiasa mkuu wake, Rais Kenyatta na kuunda chama kipya kutafuta urais, huku Odinga mwanasiasa mkongwe wa upinzani, akiwania sasa kwa mara ya tano, akiungwa mkono na Kenyatta.

Ruto anajiita 'hustler' (mpambanaji) amekuwa Makamu wa Rais Kenya tangu 2013 hadi sasa katika serikali ya Rais Uhuru Kenyatta, ya chama tawala cha Jubilee, ambaye uhusiano wake na bosi wake unazidi kudorora, chanzo cha mkwaruzano huo hakijulikani wazi duru za kisiasa zikidai mwanzo wake ni Rais Kenyatta kufikia makubaliano ya kuleta maridhiano ya kitaifa na kiongozi wa upinzani Raila Odinga, kwa lengo la kumaliza uhasama wa kisiasa.





Gideon Moi (kushoto) na William Ruto wamekubaliana kwenda pamoja. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Miaka ya hivi karibuni, Raila Odinga maarufu 'Baba' kama anavyoitwa na wafuasi wake, amekuwa na uhusiano wa karibu kisiasa na Rais Kenyatta ambaye zaidi ya mara moja amedokeza hadharani ni upande gani kisiasa anaegemea kati ya Raila Odinga na naibu wake William Ruto bila ya kutaja jina la yeyote.

Mshirika wa Odinga kisiasa katika uchaguzi uliopita alikuwa Musalia Mudavadi wa chama cha Amani National Congress (ANC), pia ambaye ameshadokeza mapema nia ya kuwa rais wa tano wa Kenya katika uchaguzi huo.

Si hao tu kuna wengine viongozi nguli wakiwania mamlaka hayo, akiwamo Gavana wa Makueni Profesa Kivutha Kibwana, makamu wa rais mstaafu Kalonzo Musyoka na mwimbaji wa muziki ya Injili Reuben Kigame.

Mara kadhaa, Musalia ameishambulia serikali ya Kenyatta kwa kushindwa kuinua uchumi wa taifa, hivyo kuyafanya maisha ya Mkenya wa kawaida kuwa magumu.

Musalia na Ruto ndiyo viongozi pekee wa siasa ambao wamekuwa wakifanya kampeni wakitangaza kuinua uchumi wa taifa, ingawa Ruto hivi Sasa ni sehemu ya Jubilee, anayeishambulia serikali ya Kenyatta kwa kushindwa kuboresha maisha ya Mkenya.

### ULIVYO MUUNGANO

Vyama vya Amani National Congress (ANC) cha Musalia Mudavadi, United Democratic Alliance (UDA), cha Ruto na kile cha Ford Kenya cha Moses Wetangula vimeamua kushirikiana kwenye uchaguzi mkuu.

Mwezi uliopita , akizungumza kwenye kongamano la Wajumbe la Taifa, la ANC, Ruto anathibitisha kuwa vyama hivyo vitashirikiana kwa maslahi ya taifa.

Kiongozi wa chama cha Wiper (soma waipa), Kalonzo Musyoka na mwenzake wa KANU Gideon Moi, wametangaza kutalakiana na Musalia baada ya kugundua kuwa Ruto ambaye ni hasimu wao kisiasa, alikuwa amealikwa kuwa mgeni wa heshima kwenye kongamano la wajumbe wa ANC, ishara ya mgawanyiko kwenye muungano huo.

"Nataka kuthibitisha kwa niaba ya UDA na wafuasi wangu, kuwa tutafanya kazi pamoja na ANC, Ford Kenya na vyama vingine vyote, kwenye safari hii ya kuleta umoja nchini Kenya," anasema Ruto.

Muda mfupi baada ya ndoa ya Kenya Moja kuvunjika, Kalonzo na Gideon kwenye taarifa kwa vyombo vya habari, wamesema huu ni wakati wa kusitisha ushirikiano wao wakiutaja kuwa ni mchezo mchafu wa siasa. Imebainika kuwa Musalia, Ruto na Wetangu'la wamekuwa wakishauriana kwa wiki kadhaa kuhusu ushirikiano mpya.

Ushirikiano huo mpya sasa unajenga jukwaa la washindani wawili wakuu kwenye uchaguzi wa Agosti 9, mwaka huu. Hata hivyo haijabainika ni nani atakayepeperusha bendera ya ushirikiano huo mpya dhidi ya Raila Odinga wa Azimio la Umoja. Raila alitajwa kuwa mradi wa serikali uliobuniwa baada ya salamu za heri.

"Sasa narudia ili kuondoa shauku, msimamo wa ANC kuhusu hiki kichekesho kinachoitwa Azimio ni kuwa hatutashirikiana nacho. Azimio limejengwa kwa maslahi ya watu wachache," anasema Musalia, ambaye pia alilaani siasa za usaliti dhidi ya Raila, anaonekana kuwasaliti wenzake ambao duru zinasema, watajiunga na Azimio la Umoja linaoongozwa na Raila Odinga.

### RUTO APUMUA

Wiki iliyopita Muungano wa Kenya-One Kenya Alliance (OKA) , ulitangaza vigogo wake Martha Karua , Cyrus Jorongo na motto wa Rais Moi Gideon Moi pamoja Kalonzo Musyoka kuungana na UDA cha Makamu wa Rais William Ruto . baada ya kumtimua Musalia Mudavadi.

Hata hivyo Jirongo ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa KANU, aliwahi kumponda Ruto akisema harakati za kisiasa kati yake na MUdavadi ambaye amemkimbia zililenga kuendeleza masuala binafsi nasi kwa manufaa ya Wakenya . Aliyasema hayo kwenye mkutano wa kampeni uliomshirikisha kiongozi wa chama cha Wiper Kalonzo Musyoka na Gideon Moi Mwenyekiti wa KANU.

## WAZIRI MKUU BORISS JOHNSON

# UINGEREZA WAAMSHA 'DUDE', KISA MISURURU YA TAFRIJA 'HARAMU'



**Na GAUDENSIA MNGUMI**

MOJA ya sheria za Chama cha Conservative cha Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson (pichani), inaelekeza kuwa kura ya kukosa imani na kiongozi wa chama inawezeshwa na wabunge 54 wa chama, iwapo wataandika barua kwa ofisa wa chama kupendekeza kupigwa kura hiyo, ili kumtumbua.

Licha ya kuwapo kwa misukosuko Conservative yenye wabunge 359, haijakusanya barua 54 za wabunge za kutaka Johnson atimuliwe.

Kinachomuweka kwenye hati hati Waziri Mkuu wa Uingereza mwenye majina lukuki 'Alexander Boris de Pfeffel Johnson' ni msururu wa 'karamu haramu', akila, kunywa na kujirusha pamoja na maofisa na marafika zake, wakati wa kampeni za kudhibiti COVID-19 zinazotangazwa na kusimamiwa na serikali yake, ikionekana kuwa anavunja sheria kwa makusudi.

Johnson anatetea baadhi ya kashfa zake zenye jina "partygate" au 'kashfa ya tafrija' tangu yaliporipotiwa kwenye magazeti mwishoni mwa mwaka jana kwamba ilikuwa mikusanyiko ya kazi, na taarifa za Idhaa ya Kiswahili ya DW.

Mei 2020, Johnson alipigwa picha akiwa na divai na jibini (cheese) pamoja na mke wake wa sasa Carrie na wafanyakazi wengine 20 kwenye bustani ya Downing Street, akijirusha.

Wakati anafanya hivyo Waingereza walikuwa wanatekeleza sheria ya kuvaa barakoa, kuzingatia umbali wa zaidi ya mita moja kati ya mtu na mtu na kuepuka mikusanyiko.

Aidha, Mei 2020 Msaidizi Mkuu wa Johnson, Martin Reynolds alituma mwaliko wa email kwa wafanyakazi ikisema ni "kunufaika vyema na hali ya hewa na kuwa na vinywaji wakizingatia vigezo vya kuweka umbali katika bustani jioni hiyo".

Kituo cha ITV News, ambacho kilipata barua pepe hiyo ya mwaliko, kilisema wafanyakazi 40 walihudhuria sherehe hiyo kwenye bustani jioni hiyo, wakila chakula na kunywa.

**KUATHIRIKA CORONA**

Machi 2020, Waziri Mkuu Johnson aliambukizwa corona akionyesha dalili za mwanzo hasa homa kali na kikohozi, hata hivyo DW ilisema licha ya kujitenga aliendelea kuongoza serikali kutoka nyumbani kwake na juhudi zilikuwa ni namna ya kupata majibu ya kukabiliana na janga la virusi hivyo, ambavyo wakati huo lilikuwa likitishia maisha Ulaya , Marekani na Asia.

Johnson ameonekana katika sherehe nyingi kuanzia Novemba na Desemba 2020, kwa mujibu wa ripoti kadhaa Waziri mkuu huyo wa Uingereza na mkewe Carrie wamehudhuria sherehe mbali mbali licha ya baadhi ya wafanyakazi wake kueleza masikitiko kwamba mikusanyiko hiyo ilikiuka udhibiti wa COVID-19.

**CHAMA KINAMBANA**

Mbunge wa Conservative wiki iliyopita 'aliamsha tena dude' akimtaka Johnson. Kwa mujibu wa BBC ni Waziri wa zamani wa Kusimamia Shule, Nicolas Gibb au Nick Gibb, ambaye hivi karibuni zaidi amewasilisha barua ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu.

Anasema wapiga kura wake walikuwa na hasira kwamba kiongozi mkuu amekuwa "akipuuza waziwazi" sheria za COVID walizoweka wenyewe.

Wakati huohuo, gazeti la Daily Mirror linaripoti kuwa picha ya Johnson akiwa ameshika bia kwenye sherehe tafrija ya kuzaliwa kwake imekabidhiwa polisi wanaochunguza ukiukaji wa sheria za corona.

Picha hiyo ni moja ya 300 zilizowasilishwa kwa uchunguzi wa polisi wa London kuhusu madai ya mikusanyiko 12 ya kujirusha kipindi cha karantini ya corona.

BBC inasema picha zinadaiwa zilichukuliwa na mpiga picha rasmi wa Waziri Mkuu, ambaye ni mtumishi wa umma, anayelipwa na walipa kodi.

Picha hiyo inamuonyesha Waziri Mkuu akiwa ameshikilia bia katika hafla iliyofanyika kwenye ofisi ya Baraza la Mawaziri, Juni 2020, pamoja na Kansela Rishi Sunak, ambaye alikuwa ameshikilia kinywaji laini.

Wakati hayo yakijiri sheria zilipiga marufuku mikusanyiko ya zaidi ya watu wawili ndani ikiwa ni jitihada za kupambana na corona.

Hilo linawadia mwishoni mwa wiki ambayo imekuwa ngumu kwa Waziri Mkuu ambapo hadi kufikia sasa wasaidizi watano wa Baraza la Mawaziri wamejiuzulu na kuchapishwa kwa matokeo ya awali ya ripoti ya Sue Gray ya matukio yaliyotokea wakati vikwazo vya COVID-19 vimewekwa.

Akiandika katika gazeti la Daily Telegraph, waziri mstaafu Gibb, ambaye ameshika wadhifa huo chini ya mawaziri wakuu watatu na ambaye alipoteza nafasi yake kama waziri wa shule katika mabadiliko ya Boris Johnson, Septemba mwaka jana, anasema wapiga kura wake "walikuwa na hasira kwa sababu ya kutokuwa na msimamo mmoja".

Na kwamba "kurejesha uaminifu, tunahitaji kubadilisha waziri mkuu."Anasema masharti ya COVID-19 yaliyowekwa na Boris Johnson "yalipuuzwa waziwazi" .

Mambo yamefanyika katika ofisi ya viongozi wakuu na Waziri Mkuu hakuwa sahihi Desemba mwaka jana , alipoambia bunge kwamba hakuna tafrija yoyote.

"Baadhi wanabishana kwamba kula pipi chache na glasi kidogo za vinywaji sio sababu ya kujiuzulu. Lakini kusema ukweli ni muhimu, na hakuna mahali pengine kuliko katika Baraza la Bunge ambapo, kama mahakama ya sheria, ukweli lazima usemwe bila kujali matokeo ya kibinafsi," anaandika, Gibb.

Anasema mwenzake Tory Aaron Bell "ameshangaza sana" alipomkosoa Johnson kuhusu karamu zilizofanywa wakati kuna vikwazo vya corona.

Bell alikuwa amemuuliza Waziri Mkuu kama alimchukulia kama mpumbavu kwa kufuata sheria mwenyewe , ikiwa ni pamoja na kutokukumbatia familia yake kwenye mazishi ya bibi yake, au kwenda kunywa chai baada ya ibada.

Ijumaa iliyopita Bell anaonya "ukiukwaji wa uaminifu" juu ya uvunjaji wa sheria na jinsi ulivyoshughulikiwa ulifanya msimamo wa Waziri Mkuu ushindwe, kwani alithibitisha pia alikuwa amewasilisha barua ya kutokuwa na imani na Sir Graham Brady - mwenyekiti wa mwaka 2022.

Takriban wabunge 54 wanatakiwa kumwandikia Sir Graham ili kuchochea kura ya uongozi wa Waziri Mkuu kutumbuliwa.

Wabunge wengine wa Conservative wanatarajiwa kutafakari iwapo wataandika barua zao.

Mbunge wa Conservative, Andrew Bridgen alipendekeza kwamba ni wakati wa baraza la mawaziri" kuonyesha uongozi" na "kukabiliana" na suala la uongozi wa Waziri Mkuu.

Lakini mbunge mwenzake Richard Bacon alipendekeza kwamba haikuwa kwa wanasiasa kubadilisha serikali - kwa kuwa hiyo ni kazi ya wapiga kura.

Na Liam Fox, katibu wa zamani wa wizara ya biashara, alisema kuna hatari chama hicho kilikuwa kikijihusisha sana na masuala makubwa kama mfumuko wa bei, mzozo wa nishati na hali ya Ukraine.

Alikiambia kipindi cha BBC kwamba: "Kutakuwa na haja ya kumalizwa kwa suala hili na Conservative na kuna mengi ya kusema, tunapaswa kuyasema, na kuna maswali ambayo yatahitajika kujibiwa."

Johnson amewaandikia wabunge wote wa chama chake akisema amejitolea kuboresha jinsi ofisi yake inavyofanya kazi.





# Wauza vyakula na vinywaji watakiwa kuyaondoa mabanda

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Afya wa Jiji la Dodoma, Abdalah Mahia, amewataka wafanyabiashara wa vyakula na vinywaji waliovamia kwenye hifadhi za barabara na kujenga mabanda yao kuviondoa kwa kuwa vinasababisha ajali.

Mahia alitoa maelekezo hayo alipofanya ziara yake kwenye Kata ya Ipagala jijini hapa na kutoa elimu kwa wafanyabiashara hao kwa kuwa ni maeneo yasiyo rasmi kufanyia biashara.

Alisema hali hiyo inahatarisha maisha yao pamoja na wateja na mali zao na pia wanakwenda kinyume cha sheria.

"Tuheshimu mamlaka badala ya kusubiri kuvunjiwa na kupigwa faini ambazo zinazoweza kuwarudisha nyuma kibiashara, mimi niwaombe tu wafanyabiashara kuheshimu mamlaka, sheria na kanuni waache kuvamia kwenye maeneo yaliyotengwa kuwa wazi, ukizingatia kuwa yanaweza kuwahatarisha biashara zao na hata kwa wateja pindi inapoweza kutokea ajali ya aina yoyote," alisema.

Mahia alisema serikali haina nia mbaya na wafanyabiashara ila kinachotakiwa kuona biashara zinafanyika kwenye maeneo yaliyotengwa ambayo ni rasmi na siyo yaliyozuiliwa na mamlaka husika.

"Hatutaki kuwavunjia mabanda yenu na kuwapiga faini, tunataka kuwaona wafanyabiashara mama na baba lishe, wakiboresha biashara kwa kuzingatia afya ya mazingira, hivyo kwa upande wao wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanajilinda wao wenyewe pamoja na wateja wao," alisema.

# Waziri awaonyesha pa kwenda waliokosa haki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, George Simbachawene, amewataka wananchi wanaohisi ndugu zao wamekosa haki na kuonewa ambao wapo mahabusu na magerezani kwenda katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kupata msaada wa kisheria.

Akizungumza na waandishi wa habari alipotembelea ofisi za tume hiyo jijini hapo, Simbachawene, alisema kazi ya tume hiyo ni kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi ili wapate haki zao za msingi za kisheria na asingependa kuona watu wanaishia kulalamika mitaani kukosa haki.

"Tume ipo na kazi yake ni kutoa msaada wa kisheria kwa taasisi, mtu mmoja mmoja, hivyo wananchi kuanzia leo mjipange kwenda tume kupata msaada wa kisheria ambao utawasaidia kujua nini wafanye ili wapate haki zao."

"Nawaomba muitumie tume kuhakikisha mnasaidiwa masuala ya kisheria ili muweze kuendelea na shughuli zenu za kila siku," alisema Simbachawene.

Alisema amekuwa akisikia malalamiko mengi, mitaani, mauaji, kukosa haki polisi, mahakamani vyote hivyo ni kazi ya tume kutoa elimu ya kisheria ili watu wajue.

Aliwataka viongozi wa serikali kuwaelekeza watu wenye kero mbalimbali kutambua umuhimu wa chombo hicho.

Alisema kuanzia sasa anahitaji kuona chombo kinakuwa maarufu kwa kujitangaza, huku akivitaka vyombo vya habari kusaidia kutoa taarifa ili wananchi waitumie tume hiyo kutatua kero mbalimbali.

Akizungumzia kuhusiana na Ripoti za Tume hiyo kufikishwa bungeni, Waziri Simbachawene aliahidi kuanzia sasa ripoti hizo zitafika na kusomwa bungeni kama zilivyo ripoti za taasisi nyingine.


"Niwahakikishie mimi kama waziri mwenye dhamana, kama ripoti mnazo leo basi kesho zitazifikisha bungeni ili zisomwe," alisema Simbachawene.

Alisema tume hiyo inapaswa kujulikana na kuwa maarufu kwa sababu inafanya kazi za kutafuta haki za binadamu ambao wanahitaji msaada wa kisheria.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, alisema tume hiyo imefurahishwa na serikali kuwaongezea bajeti kutoka Sh. bilioni moja hadi tatu huku akidai kuwa bado hazitoshi mahitaji.

Alisema zinahitajika Sh. bilioni sita ili kukidhi mahitaji na kufikia maeneo ambayo hawayafikii kwa ajili ya kutatua kero za wananchi.

Jaji Mwaimu aliomba serikali kuongeza wafanyakazi ili kuongeza nguvu ya kiutendaji katika kazi zao za kila siku ambazo wanatakiwa kufanya.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (wanne kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 817.4 kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu vilivyokopeshwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma. Wengine ni Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru (wapili kushoto), Naibu Meya wa Jiji, Emmanuel Chibago (watatu kushoto) na (mwenye tai) ni Naibu Waziri wa Kilimo, Athony Mavunde. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Asilimia 0.092 tu walioacha shule sasa warejea

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, amesema watoto 13 kati ya 14,000 ( sawa na asilimia 0.09286) walioacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupata ujauzito wamerudi shuleni.

Kutokana na hali hiyo, amewataka viongozi wa ngazi zote kuhakikisha wanafuatilia na kusimamia watoto hao kurejea shuleni ili kutumia fursa iliyotolewa na serikali.

Katibu Tawala huyo aliyasema hayo juzi kwenye hafla ya utoaji tuzo kwa wanafunzi wa mkoa huo waliofaulu vizuri na kupata daraja la kwanza la pointi za juu katika mtihani wa Taifa wa kidato cha nne wa mwaka 2021 na walimu waliofaulisha vizuri masomo waliyofundisha ambapo Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka alitoa tuzo hizo kama motisha kwao.

Dk. Mganga alisema "Tumepewa fursa ya watoto walioacha shule kurudi kwa Mkoa wa Dodoma sisi huwa tunachangamoto ya watoto kuachia masomo njiani (mdondoko), sasa tumepata fursa watoto warudi shule, lakini hadi wiki hii iliyopita ilikuwa ni wanafunzi 13 tu waliorudi shule kati ya 14,000."

"Hawa ni watoto wengi sana kama watoto wa 'form two' tu walioacha kufanya mtihani waliodondoka kabla ya mtihani walikuwa zaidi ya 2,400, sasa hawa watoto wamepewa fursa ya kurudi shuleni na serikali wasome, ninawaomba viongozi wenzangu tukafanyie kazi hili jambo ili watoto wetu wapate fursa ya kurudi shuleni ili kuondoa ujinga," alisema.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuondokana na tatizo la watoto wa mitaani.

"Maana ukiwaacha mitaani mtoto wa darasa la nne anakwenda wapi? Anaishia mtaani kuzurura kwa hiyo twendeni tukafanye jitihada katika hili, pia tuhamasishe watoto wenye ulemavu watolewe majumbani waripoti shuleni, na watapelekwa kwenye shule inayohusika," alisema.

Kuhusu wanafunzi wa kidato cha kwanza, Katibu huyo alisema hadi sasa asilimia 70 ya wanafunzi wameripoti huku asilimia 30 bado hawajaripoti.

Alitoa rai kwa viongozi wa wilaya kila mmoja aende kufanya jitihada ili itakapoisha wiki hii wawe wameripoti kwa asilimia 100.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema kuna barua imeandikwa na Baraza la Taifa la Mitihani kuwa wanafunzi 269 waliotahiniwa mtihani wa darasa la nne mwaka jana wamebainika hawajui kusoma na kuandika.

"Ni lazima tusimamie watoto wasome, somesha watoto wako, wapeni watoto fursa ya kusoma waingie kwenye dunia ya ushindani," alisema.

Hata hivyo, alisisitiza iwapo kuna mzazi ambaye mtoto wake hajaripoti shule hadi sasa, hatua dhidi yake zitachukuliwa kwa kuwa amedhamiria kuhakikisha watoto wa mkoa huo wanapata elimu.

"Mzazi ambaye mtoto wake hayupo shuleni sio kazi wa polisi ni mgambo na sungusungu wa eneo hilo, sasa mtakimbia nyumba zenu kwasababu anatafutwa mtoto wako kwenda shule, viongozi mpo humu kasimamieni hili, kuna wazazi wa ajabu mwingine anamshawishi mtoto kufanya vibaya ili wamwozeshe sasa hao nitakwenda nao sambamba," alisema.





# RC aagiza maeneo yote ya shule mkoa kupimwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameziagiza Halmashauri za Mkoa huo, kupima maeneo yote ya shule na kuzipatia hati miliki ili kuepusha migogoro na wananchi.

Agizo hilo alilitoa baada ya kubaini maeneo mengi ya taasisi za umma hayana hati miliki zikiwamo shule kutokana na jamii kuhamasika kupeleka wanafunzi katika shule za mchepuo wa kiingereza.

Homera alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu mikakati ya Mkoa kuinua ufaulu wa wanafunzi kwa mwaka 2022/2023.

"Katika vikao vyetu tulibaini vikwazo vingi katika sekta ya elimu miongoni ni kutopima maeneo yanayozunguka shule pamoja na kutopatiwa hati za umiliki ili kuondoa migogoro, sambamba na hilo pia ufaulu wa shule zilizopo mbali na makao makuu ya Wilaya huwagharimu watoto na kuchangia mimba pamoja na utoro," alisema Homera.

Kutokana na vikwazo hivyo aliwaagiza viongozi wa halmashauri waendelee kufanya ufuatiliaji wa maendeleo ya shule zilizopo pembezoni mwa miji sambamba na kuongeza mgawo wa walimu wa masomo ya sayansi kwa shule zilizoko nje ya miji.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alisema katika bajeti ya mwaka 2022/2023 Halmashauri ya Busokelo imetenga bajeti ya shilingi milioni 35 kwa ajili ya ujenzi wa matundu 32 ya vyoo.

Aliongeza kuwa shilingi milioni 160 zilitengwa wa ajili ya ujenzi wa vyumba nane vya madarasa ya msingi pamoja na shilingi milioni 7.5 kwa ajili ya ukamilishaji wa matundu 11 ya vyoo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa, alisema utekelezaji umefanyika ambapo ukamilishaji ujenzi umefanyika wa vyumba 67 vya madarasa na viti na meza 1,985 hadi kufika sasa.

Aidha Mlawa alishauri wadau wa maendeleo wanapotaka kutoa misaada ya kusaidia ujenzi wa miundombinu ya shule ni vyema kufika Ofisa za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili wasikinzane na taratibu za utoaji misaada.




Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Kusini, Mhandisi Boniphace Guni, akitoa elimu kwa wakazi wa Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma jana, kuhusu mifuko (vifungashio), isiyofaa kwa matumizi ya kubebea bidhaa, ili kulinda mazingira na afya za watumiaji. **PICHA: AMON MTEGA**

## TMDA kuwanoa vijana athari kutumia tumbaku

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Dawa, Vifaa na Tiba (TMDA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imesema miongoni mwa mikakati iliyopo kwa sasa ni kutoa elimu kwa vijana juu ya athari zitokanazo na matumizi ya bidhaa za tumbaku.

Kaimu Meneja wa TMDA Kanda hiyo, Anitha Mshighati, alisema miongoni mwa sera zilizoandaliwa na Mamlaka hiyo ni kuwalinda vijana walio na umri chini ya miaka 18 na watu wote wasiotumia tumbaku kutoshawishika kutumia bidhaa hizo.

Alisema watahakikisha kwamba jamii inataarifiwa juu ya madhara ya tumbaku na faida za kuacha kutumia bidhaa za tumbaku na kwamba licha ya mahitaji hayo watasimamia kuhakikisha zinatengenezwa kwa vigezo vya usalama.

"Miongozo iliyoandaliwa itasaidia kufanya kaguzi za mara kwa mara za bidhaa na kuelekeza watumiaji wa tumbaku kuvuta/kutumia katika maeneo maalumu yaliyotengwa sambamba na kukataza kuvuta katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu wengi," alisema Mshighati.

Aidha aliwataka wamiliki wa kumbi za starehe, nyumba za ibada, hospitali, majengo ya ofisi, vyuo maeneo ya soko viwanja vya ndege, stendi za mabasi na viwanja vya mipira kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya wavuta sigara.

Alitoa wito kwa Halmashauri kuzingatia kanuni za kukasimu baadhi ya madaraka na majukumu ya TMDA kwa Halmashauri kupitia GN namba 476 ya mwaka 2015 pamoja na marekebisho yake GN namba 19 ya mwaka 2017.

Alisema ukasimishaji umezingatia kifungu cha 113 (2) cha sheria ya serikali za mitaa ya Halmashauri za Wilaya kukagua maeneo yanayotoa huduma za dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

**Aidha aliwataka wamiliki wa kumbi za starehe, nyumba za ibada, hospitali, majengo ya ofisi, vyuo maeneo ya soko viwanja vya ndege, stendi za mabasi na viwanja vya mipira kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya wavuta sigara.**

## Sababu za kupungua watoto wanaozaliwa na uzito mdogo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

IDADI ya watoto waliozaliwa wakiwa na uzito chini ya kilogram 2.5 imepungua kutoka asilimia 11.7 katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 9.1 Desemba 2021.

Aidha, utapiamlo mkali umeshuka kutoka asilimia 0.7 hadi asilimia 0.6 kwa mwaka 2021,ambapo jitihada hizo zimetokana na mkataba wa lishe ambao umekuwa ukitekelezwa kwa ufanisi katika Halmashauri zote ambapo utekelezaji wake umeongezeka kutoka asilimia 72 mwaka 2018/2019 hadi asilimia 98 mwaka 2020/2021.

Kutokana na jitihada hizo, kwa mwaka 2020/2021 Mkoa wa Mbeya ulishika nafasi ya kwanza kitaifa kwa utekelezaji wa mkataba wa lishe.

Ofisa lishe wa Mkoa wa Mbeya, Benson Sanga, alisema jana kuwa mafanikio hayo yametokana na utoaji wa elimu kwa wajawazito na wenza wao ambapo kamati za lishe katika kila kijiji, mtaa na kata wanafanya kazi ya kuwatembelea wananchi kuwapatia elimu ya lishe bora kabla na baada ya kujifungua kwa siku 1,000 za mwanzo.

Sanga alisema katika kuhakikisha hali ya lishe mkoani Mbeya inakuwa vizuri na kuondokana na tatizo la udumavu, ni kufanya utambuzi wa watoto wa chini ya umri wa miaka mitano wenye utapiamlo mkali.

Alisema hali ya utapiamlo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano bado hairidhishi na kwamba katika kipindi cha mwaka 2018/2019 utapiamlo mkali ulifikia asilimia 40 na mwaka 2020/2021 hali ya utapiamlo ilifikia asilimia 96.3.

"Katika kukabiliana na tatizo la udumavu, wazazi na walezi, wenye watoto wa umri wa chini ya miaka miwili wameendelea kupewa elimu ya namna bora ya ulishaji wa watoto wao kupitia vituo vya tiba katika jamii na kwamba asilimia 99 ya wazazi walipewa elimu ya lishe na wahudumu wa afya ngazi ya jamii,"alisema Sanga.

Aliongeza kuwa Halmashauri zote zilitoa matone ya vitamin 'A' kwa wastani wa asilimia 97 kwa watoto chini ya miaka mitano vilevile asilimia 76 ya wajawazito waliohudhuria kliniki waliweza kupewa vidonge vya kuongeza damu mwilini ili kupunguza tatizo la upungufu wa damu.





## Serikali yatangaza bei elekezi sukari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetoa bei elekezi ya sukari baada ya kuwapo kwa viashiria vya baadhi ya wafanyabiashara kutaka kupandisha bei ya bidhaa hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaban, alibainisha kuwa kilo moja ya sukari itaendelea kuwa Sh. 2,000.

Waziri huyo alisema uamuzi huo umelenga kuwawezesha wananchi wenye kipato cha chini kuhimili wimbi la kupanda kwa bei za bidhaa hasa zile muhimu katika kipindi hiki ambacho imebaki miezi miwili kuingia kwenye mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Alisema serikali imepokea maombi kutoka kwa wafanyabishara waingizaji wa sukari, wakishauri serikali kufanya mapitio ya tangazo lake la bei elekezi kwa bidhaa ya sukari kutoka Sh. 2,000 kwa kilo hadi Sh. 2,300 kutokana na gharama za uagizishaji wa bidhaa hiyo kupanda katika soko duniani.

Shaban alisema serikali baada ya kutafakari maombi hayo imeona ni vyema bei elekezi ikaendelea kubaki kama awali lakini kwa kuwa hoja iliyotolewa na wafanyabishara ya kutaka kuongeza bei ni ya msingi, serikali imeamua kupunguza ushuru wa uingizaji wa sukari kwa asilimia 50 ili kupunguza gharama ya kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

"Serikali imeamua kujinyima mapato yanayotokana na ushuru wa kuagiza bidhaa hiyo ili wananchi waendelee kupata bidhaa hiyo kwa bei nafuu na haitakubali kuona wananchi hawanufaiki na punguzo hilo la ushuru na badala yake wafanyabishara wanafaidika zaidi," alionya.

Alisema wizara itaendelea kufuatilia mwenendo wa bei ya sukari duniani kwa lengo la kusimamia ipasavyo bei elekezi ambazo imekuwa ikitoa mara kwa mara.

Waziri huyo alitoa miezi mitatu kwa wafanyabishara ambao wamepewa kibali cha kuingiza sukari na hawajaingiza sukari karibu mwaka mzima, kuwanyang'anya vibali hivyo endapo watashindwa kuingiza sukari.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wafanyabishara katika Soko la Darajani waliipongeza serikali kwa uamuzi wake huo wa kushusha ushuru kwa asilimia 50 katika uingizaji wa bidhaa hiyo.

"Tunaipongeza serikali kwa hatua hiyo maana kipindi hiki cha kuelekea Ramadhani mahitaji ya sukari huwa makubwa kwa hiyo tutauza kwa bei elekezi iliyowekwa na serikali," alisema Khamis Ali, mfanyabiashara wa eneo hilo.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi wameiomba serikali kusimamia bei ya mafuta ya kula kama walivyofanya kwa sukari maana bado bei ya bidhaa hiyo ipo juu.

# DPP ashtukia kesi kukomoana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mashtaka Zanzibar (DPP) Salma Hassan, amesema kutokana na serikali kufuta dhamana kwa washtakiwa wa kesi za udhalilishaji kumekuwa na viashiria vya raia kubambikiana kesi za udhalilishaji kwa nia ya kukomoana na kulipizana visasi au kwa kuzigeuza kesi hizo kuwa vitega uchumi.

Amesema wananchi wanaitwisha mzigo mkubwa wa kesi Ofisi ya DPP na kukataa kutoa ushahidi hasa katika kesi za udhalilishaji, akisisitiza kuwa limekuwa 'donda sugu' linalohitaji mabadiliko ya kisera na kisheria.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Sheria yaliyofanyika mjini Zanzibar juzi, Salma alisema serikali ilikuwa na dhamira nzuri ya kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya udhalilishaji kwa kufuta dhamana kwa washtakiwa wa kesi hizo, lakini kwa sasa inapaswa kuja na mikakati mipya katika eneo hilo hasa kwa watoto wa kike kuanzia miaka 14 hadi 17.

DPP Salma alisema rasilimali na muda ambao hutumika katika mashauri hayo ambayo huishia kuondolewa mahakamani kwa kukosekana mashahidi au mashahidi wanapofika mahakamani kwa makusudi kuwakataa wahusika ilhali wao wenyewe waliwataja vituo vya polisi wakati wakitoa maelezo yao, utumike katika mambo mengine ya utoaji wa haki wenye tija kwa taifa.

"Kaulimbiu yetu Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni hakuna hatia bila ya ushahidi, usidharau, usikatae kutoa ushahidi," alisema.

DPP alisema ofisi yake imeelewa dhamira ya Rais Dk. Hussein Mwinyi ya kutaka kuiona Zanzibar inapata maendeleo ya kiuchumi kwa kutilia mkazo dhana ya uchumi wa bluu ambao unaenda sambamba na ustawi wa jamii kwa kuangalia nafasi za wanawake na kuwalinda watoto ambao ndio waathirika wakubwa katika matendo ya kijinai.

Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Abdallah Ramadhan, alisema mahakama imeweka mahakimu maalumu wa kusikiliza kesi za udhalilishaji ili uamuzi wa kesi hizo kusikilizwa na kutoa hukumu kwa haraka.

Alibainisha kuwa kuna ongezeko kubwa la mahabusu katika magereza, hivyo aliwaagiza mahakimu kwa zile kesi ambazo sheria zinaruhusu dhamana kuwapa dhamana watuhumiwa na zile kesi ambazo hazina dhamana, kuongeza nguvu kutoa uamuzi kwa haraka ili wenye hatia watumikie vifungo vyao na wasio na hatia waachiwe ili kushiriki katika shughuli za ujenzi wa uchumi wa nchi.

Akizungumzia kuhusu kukwama kwa kesi za udhalilishaji, alisema mahakamani hakuna tatizo la ushahidi kwa kesi za ubakaji kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 14 katika kutoa ushahidi lakini tatizo lipo kwa watoto wa kike wanaobakwa wenye miaka 15 hadi 17.

"Mashahidi ambao hawafiki mahakamani kwa kesi za udhalilishaji ni hawa wahanga wenye umri wa miaka 15 hadi 17 na hasa wale ambao watuhumiwa wanatuhumiwa kufanya makosa ni wenzao wenye miaka 18 hadi 22, hapa ni tatizo," alifafanua.

Alitoa mfano kwamba Mahakama ya Wete Pemba kuna mwathirika wa kesi za udhalilishaji amewaweka vijana watatu gerezani kwa madai ya kudhalilishwa, lakini ushahidi unasuasua.

Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi, alisema kuwa wakati serikali inaamua kutengeneza sheria ya kuondoa dhamana kwa watu wanaofanya udhalilishaji, ilikuwa na lengo la kumaliza vitendo hivyo katika jamii ambavyo vimekithiri.



Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, Khatib Juma Mjaja (kushoto), akikabidhi madawati kwa Kaimu Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, Halifa Bakar Waziri, wilayani humo jana, kwa ajili ya madarasa yaliyojengwa na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla (hayupo pichani), katika shule ya Kiwani. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Tende tani 29 zateketezwa Z'bar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BODI ya Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA) imeteketeza tani 29 za tende zilizomaliza muda wake wa matumizi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya uteketezaji wa bidhaa hiyo katika jaa kuu la Kibele, Wilaya ya Kati Unguja, Mkaguzi Mkuu wa Chakula na Utekelezaji, Suleiman Akida Ramadhani, alisema jana kuwa tende hizo zilizomaliza muda wake zimegundulika katika ghala lisilo rasmi lililoko Kilimahewa mjini Unguja.

Alisema tende hizo ziligundulika baada ya wananchi wa eneo la karibu na ghala hilo kubaini harufu na nyingine kutupwa mitaani katika sehemu za Welezo na kupeleka taarifa kunakohusika na kuchukuliwa hatua za haraka.

Mkaguzi huyo alisema iko haja ya kutolewa elimu kwa wafanyabiashara wanaoleta bidhaa zilizokuwa zimeshamaliza muda wake, kuacha tabia hiyo kwa sababu zinaathiri jamii inayotumia bidhaa hizo.

Alisema bidhaa hizo zinapotumika zinaathiri afya ya mlaji kwa kemletea madhara makubwa mwilini.

Ofisa Mazingira kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Mambo ya Hali ya Hewa, Lailati Mussa Foum, alisema bidhaa zilizoharibika zinahitaji kuteketezwa kwa haraka na siyo sahihi kutumika kwa jamii.

Alisema wafanyabiashara wahakikishe wanaleta bidhaa zilizo salama kwa matumizi, ziwe na viwango na iwapo zitagundulika kubakia muda mfupi wa matumizi, zisiingizwe nchini.

Wananchi waliishukuru bodi kwa kuchukua hatua za haraka kuteketeza bidhaa hiyo, ikizingatiwa mwezi mtukufu wa Ramadhani unakaribia, hivyo kulikuwa na hatari ya kutumika.

HABARI KITAIFA

# Bunge latoa mbinu kukabili utakatishaji

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeitaka serikali kutunga sera, mbinu na mifumo ya utakatishaji wa fedha haramu, ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji Fedha.

Vilevile, limeshauri makosa makubwa ndiyo yatakayotambuliwa kuwa ni ya ugaidi huku kukiwa na watu binafsi ambao watatangazwa kuwa magaidi wa ndani na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Wakichangia muswada huo, baadhi ya wabunge walitaka haki itendeke kwa wanaokamatwa kwa tuhuma za ugaidi na kutoa elimu kwa umma ili kuepusha watu kuumizwa.

Makamu Mwenyekiti, Omari Kigua, akiwasilisha maoni ya kamati hiyo, alisema inakubaliana na dharura na uhitaji wa Sheria ya Kudhibiti Ugaidi nchini na kwamba sera iwe na malengo, dhima na dira inayoendana na sheria iliyoko.

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji Fedha Haramu wa Mwaka 2022 uliwasilishwa bungeni jana kwa hati ya dharura.

"Tafsiri iliyoko hivi sasa kwenye sheria ilikuwa haiweki tofauti ya kitendo na nia ya kuwatambua magaidi binafsi. Sheria ilivyo kwa sasa inatambua vikundi vya kigaidi tu. Kuweka utaratibu wa kisheria wa kutangaza magaidi wa ndani ya nchi kupitia waziri mwenye dhamana ya masuala ya mambo ya ndani ya nchi.

"Baada ya majadiliano na serikali, kamati iliishauri na ikakubali kuongeza maneno 'seriously' (makosa makubwa) ili kuondoa makosa mengine ya kawaida yasije yakatafsiriwa kama makosa ya kigaidi.

"Kimsingi mapendekezo haya yanaendana na Tamko la Kimataifa la Kuzuia Ufadhili wa Ugaidi la Mwaka 1999 ambalo Tanzania imeridhia," alisema.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, mabadiliko yanayofanyika, yana lengo la kuifanya nchi iendane na mabadiliko ya kimataifa na kuondoa mwanya wa nchi kutumika kama eneo oevu la kutakatisha fedha na kufadhili ugaidi.

Awali, akiwasilisha hoja, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema lengo la muswada huo ni kuondoa dosari na upungufu uliobainishwa katika Ripoti ya Tathmini ya Tanzania ya mifumo ya nchi ya udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

"Tathmini hiyo ilifanywa na Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika wa Kupambana na Utakatishaji wa Fedha Haramu Mwaka 2021 ambayo Tanzania ni mwanachama.

"Matokeo ya tathmini yalibainisha upungufu katika sheria hii unaotokana na mabadiliko ya viwango vya udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi pamoja na matumizi ya teknolojia mpya katika uhalifu," alisema.

Waziri huyo alisema serikali imekubali marekebisho kuwa makosa yawe ni makubwa ili kuendana na mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia na kwamba wamejumuisha gaidi binafsi na siyo taasisi pekee.

Muswada huo unapendekeza adhabu ya fedha kwa anayekiuka sheria kwa kampuni au taasisi ambayo ni Sh. milioni 500 au mara tatu ya kiwango cha fedha kilichohusika katika kosa na kwamba wahusika ni watendaji wakuu wa maeneo hayo.

Waziri huyo alisema sheria inampa mamlaka Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kutunga kanuni katika maeneo yaliyoainishwa kwenye sheria hiyo.



Wafanyabiasharawamahindimabichi, wakifanyashughulizaojiraninamaji taka yaliyotuamakatikasoko la Mawasiliano, ManispaayaUbungo, mkoani Dar es Salaam hivi karibuni, kitendokinachohatarishausalamawaafyazao. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Dar yaongoza kwa visa vipya corona

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MKOA wa Dar es Salaam umetajwa kuongoza kwa idadi kubwa zaidi ya waliothibitika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO-19 ukiwa na wagonjwa wapya 184 kati ya visa vipya 252 vilivyoripotiwa.

Visa hivyo vimeripotiwa katika kipindi cha Januari 29 hadi Februari 6, mwaka huu, huku wagonjwa wapya 76 kati ya 78 waliolazwa wakiwa ni wale ambao hawajachanjwa na vifo vilikuwa vitatu.

Kutokana na hali hiyo, Wizara ya Afya imewataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo ikiwamo kuchanja chanjo ya UVIKO-19.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, visa hivyo vipya ni kati ya watu 8,529 waliopimwa katika kipindi hicho, sawa na asilimia tatu.

"Tangu ugonjwa huu ulivyoripotiwa kwa mara ya kwanza hapa nchini mnamo Machi 2020 hadi kufikia Februari 6, mwaka huu, jumla ya watu 33,482 walithibitika, sawa na asilimia 7.6 kati ya 442,566 waliopima na jumla ya watu 792 wamepoteza maisha," alibainisha.

Aliongeza: "Kwa siku ya Februari 6, mwaka huu, wagonjwa mahututi tisa waliripotiwa na wote walikuwa ambao hawajachanja chanjo ya UVIKO-19 na mgonjwa mmoja ameripotiwa kuwa kwenye mashine ya kusaidia kupumua na alikuwa hajachanjwa."

Mganga huyo alisema vifo vitatu vilivyotokea kwa kipindi hicho katika mikoa ya Dodoma, Morogoro na Manyara na vyote vilikuwa vya wagonjwa ambao hawajachanjwa.

Alisema serikali imeendelea kutoa huduma za chanjo nchini ili kuwezesha wananchi kupata kinga dhidi ya ugonjwa huo ambapo hadi Februari 6, mwaka huu dozi 9,845,774 za chanjo zilikuwa zimepokewa nchini.

"Tangu kuanza kwa zoezi la uchanjaji nchini mpaka kufikia Februari 6, mwaka huu jumla ya watu 2,117,387, sawa na asilimia 3.67 wamepata dozi kamili ya chanjo," alisema.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanapata dozi kamili za chanjo, kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kuvaa barakoa kwa usahihi, kuzingatia usafi binafsi kwa kunawa mikono, kuwahi kwenye vituo vya afya wanapohisi dalili za ugonjwa huo na kuzingatia kufanya mazoezi.

## Wizara yajipa hadhari utekelezaji wa miradi

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

WIZARA ya Nishati imesema ina jukumu kubwa la kusimamia miradi mikubwa saba kati ya 17 ya kimkakati ikiwamo ya kuzalisha umeme wa Bwalo la Nyerere, Bomba la Mafuta, Nishati Vijijini na usambazaji wa gesi, ikitahadharisha kuwa isipoitekeleza kwa ufanisi, itaiangusha mipango yote mikubwa inayoendelea kutekelezwa nchini.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, alisema hayo jana mjini Morogoro baada ya kukutana na wafanyakazi wa wizara hiyo kwenye mkutano wa Baraza la Wafanyakazi.

Alisema Watanzania wana matarajio makubwa kutoka kwenye wizara hiyo kutokana na majukumu makubwa iliyopewa.

Aliwataka watumishi wa wizara hiyo kuacha kufanya kazi kwa mazoea badala yake wazingatie sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya serikali inayotolewa kila baada ya muda katika utendaji wao wa kazi ili kuongeza ufanisi na kutii kiu ya matarajio ya Watanzania.

"Mnatakiwa kujifunza kufanya kazi kwa ubunifu zaidi na kuongeza kazi katika utekelezaji wa majukumu yenu, endeleeni kujituma kwa weledi na uadilifu ili kuongeza ufanisi wa kazi, wananchi wa Tanzania wana matarajio makubwa na Wizara ya Nishati na matarajio hayo yanatokana na ukweli kwamba tumebeba jukumu kubwa la kiutendaji," alisema.

Alisema dhamana ya miradi hiyo mikubwa wanayoisimamia ni karibu asilimia zaidi ya 40 ya mipango yote ya nchi ndio maana wizara isipotekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi kama inavyotakiwa, mipango yote iliyowekwa itaanguka.

"Mimi kama mtendaji mkuu wa wizara nitahakikisha nasimamia miradi yote kikamilifu na kwa bidii ili miradi saba ya kimkakati itekelezwe kulingana na matarajio ya taifa, ndio maana mabaraza haya ya wafanyakazi ni muhimu, yanasaidia kukumbushana juu ya wajibu wetu kama wafanyakazi na kutoa mchango kwa kadri inavyotarajiwa," alisema.

Kuhusu mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaogharimu Sh. trilioni 6.5 hadi kukamilika, alisema hadi sasa jumla ya Sh. trilioni 3.4 zimelipwa kwa mkandarasi wa mradi huo Arab Contractors and Elsewedy Electric kutoka Misri na hakuna deni lolote linalodaiwa katika kazi zilizokwishafanyika.

Alibainisha kuwa hadi sasa maendeleo ya mradi huo ni mazuri na umefikia asilimia 55 ya utekelezaji wake na kwamba mpaka kufikia mwisho wa Januari mwaka ambapo wameendelea kufuatilia kwa ukaribu zaidi kutokana na manufaa yake makubwa yanayotarajiwa kupatikana kutoka kwake ikiwamo ajira na uhakika wa upatikanaji wa nishati nchini.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE) Tawi la Wizara ya Nishati, Ziambwe Chinula, alisema wafanyakazi wanajivunia mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa na wizara hiyo ikiwamo kuongeza uzalishaji wa umeme, kuunganisha magari zaidi ya 7,500 na mfumo wa gesi na kuokoa zaidi ya Sh. milioni 462 kila mwaka.

HABARI MICHEZO

# SIMBA, PRISONS ZATOA NENO GSM KUJITOA UDHAMINI LIGI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU za Simba na Tanzania Prisons zimekuwa za kwanza kuongea baada ya mdhamini mwenza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kampuni ya GSM kujiondoa kudhamini kwa sababu mbalimbali ilizotaja juzi, ikiwamo kutotekelezwa kwa baadhi ya vipengele vya mkataba huo.

Wakati Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu ya Simba, Ahmed Ally akisema kuwa klabu yao tangu mwanzo waliona mkataba huo haukuwa na viashiria bora kwenye maslahi ya mpira na walijaribu kupambana, lakini klabu zingine hawakuwaelewa, Prisons imesema kujiondoa kwake ni pigo kubwa kwenye soka la Tanzania.

"Haki imeshinda, ndivyo ninavyoweza kusema, Simba hatukukubaliana na ule mkataba kwa sababu tangu mwanzo tuliona hauna viashiria bora kwenye maslahi ya mpira wetu, tulijaribu kupambana lakini kwa bahati mbaya wenzetu hawakutuelewa, kwa maana ya klabu zingine, wao waliosimama kwenye upande wao, sijui niseme ni woga au nini, lakini Simba tulisimama na kuonyesha ujasiri na uelewa wetu kwenye mambo ya mkataba. Wakati ule klabu na mamlaka husika hazikutuelewa, hatimaye wamekuja kutuelewa sasa, ndiyo maana tunasema haki imeshinda," alisema Ahmed.

Alilipongeza Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa kupambana kuziletea klabu wadhamini kwani wakati mwingine hilo siyo jukumu lao peke yao, kwani klabu nazo zina wajibu wa kutafuta wadhamini, ila imekuwa ngumu, lakini pamoja na yote hayo ugumu huo usitumike kama fimbo ya kuleta kila aina ya wadhamini, na pia kuwe na dhana na ushirikishwaji.

Katibu Mkuu wa Prisons Antony Hau, kwa upande wake ameonyesha kusikitishwa kwa GSM kujiondoa kwenye udhamini wa Ligi Kuu, akisema ni pigo kubwa kwenye soka la Tanzania.

"Mdhamini anapoondoka tunapungukiwa kwa sababu kuondoka kwake kunapunguza baadhi ya vitu ambavyo tulitarajia kuvipata.

"Kuendesha soka na kugharamia wachezaji ni kazi kubwa, ukweli ni kwamba kwenye soka la sasa mdhamini ni mtu muhimu sana. Tutaongea kwenye vikao vyetu ili tujue ni nini kimetokea, lakini hili ni pigo kwani maisha ya sasa ya soka yanategemea sana wadhamini," alisema.

Hata hivyo, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limekiri kupokea barua kutoka Kampuni ya GSM kujitoa katika orodha ya wadhamini wa Ligi Kuu, na kueleza kwamba litaifanyia kazi kabla ya kutoa majibu.

TUNAMINYWA...



Ofisa Habari wa Yanga, Haji Manara, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kutoridhishwa na maamuzi ya waamuzi wanaochezesha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kile alichoeleza kuwa wanaiminya timu hiyo. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Biashara yafunguka sakata Nkane, Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Biashara United imekanusha taarifa zinazosambazwa kwenye mitandao ya kijamii zikimhusisha aliyekuwa mchezaji wao, Denis Nkane na Kampuni ya GSM, ikidai ni za uongo na hazijatolewa na wao, huku ikisikitishwa na upotoshaji unaosambazwa na watu wenye nia ovu juu kutokamilika kwa malipo ya kuwauzia mchezaji huyo.

Taarifa rasmi iliyotolewa kwa umma na klabu hiyo jana, imeeleza kuwa haihusiki kwa namna yoyote ile na taarifa hiyo na wameviarifu vyombo husika ili hatua zaidi za kisheria zichukuliwe kwa yeyote atakayebainika kusambaza habari hizo ambazo hazina nia nzuri juu ya mchezaji huyo, klabu na Kampuni ya GSM.

"Uongozi wa Biashara United unasikitishwa na upotoshaji unaosambazwa na watu wenye nia ovu juu ya aliyekuwa mchezaji wetu, Denis Nkane na GSM.

Hatuhusiki kwa namna yoyote ile na taarifa hiyo na tumeshatoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika kwa hatua zaidi za kisheria kwa yeyote atakayebainika," iliandikwa taarifa hiyo kwenye mtandao wa Instagram wa klabu hiyo.

Kumekuwa na taarifa inayozunguka kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha kuwa imetolewa na klabu hiyo juu ya mchezaji Nkane aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili, kuwa kampuni hiyo, inayoifadhili Klabu ya Yanga haijamaliza deni la pesa za usajili wake, kitu ambacho Biashara imekanusha vikali.

# Mdundo mtandaoni yakua asilimia 22

**Na Mwandishi Wetu**

HUDUMA ya utiririshaji wa muziki wa Kiafrika, Mdundo, imetangaza ukuaji kwa asilimia 22 kwa watumiaji wake kwenye nusu ya mwisho wa mwaka 2021.

Jukwaa hilo lilirekodi watumiaji milioni 20 mwishoni mwa robo ya mwaka (Q4), ikipanda kutoka watumiaji milioni 16.3, ikichangiwa na uhitaji mkubwa wa huduma ya muziki iliyo rahisi kutumia, pamoja na upanuzi mkubwa katika maeneo mapya barani Afrika.

Rachel Karamu, Mkuu wa Mdundo, alimwambia mwandishi wetu jana kuwa kampuni hiyo inaona ukuaji huu endelevu umechangiwa na ushirika wenye nguvu kati yake na kampuni za mawasiliano pamoja na chapa zinazoongoza kwa walaji kama MTN Nigeria, Vodacom Tanzania, Guinness, SportPesa na Standard Chartered Bank, hivyo kushuhudia huduma hii ikiongeza watumiaji wake kwa wingi, soko la kipato cha kati, hasa kati ya eneo la umri wa miaka 18-24.

"Tumebaini ongezeko la uhitaji wa huduma ya muziki inayotolewa mtandaoni, hasa miongoni mwa kundi la watumiaji vijana, walaji wanaofuatilia kikamilifu kuona bidhaa mpya na suluhu za kuunga mkono mfumo wao wa maisha," alisema Karanu.

Alisema ongezeko lililoonekana dhahiri lilirekodiwa Tanzania, Nigeria na Kenya, ikichochewa na kuongezeka kwa umaarufu wa jukwaa hilo, hasa miongoni mwa kundi la umri kati ya miaka 18-24.

Aidha, alisema jumla ya watumiaji wa kipekee Q4 kwenye masoko hayo matatu sasa wanafikia milioni 12.1; Tanzania ikiwa na milioni 3.7, Kenya milioni nne na Nigeria milioni 4.4. masoko mengine makubwa kwa Mdundo ni pamoja na Uganda (milioni 1.8) na Ghana (milioni 1.6), huku Mdundo kwa sasa ikijivunia kuwa na watumiaji milioni 13.3 kwa mwezi barani Afrika.

Alisema Mdundo inatazamia ukuaji endelevu zaidi kupitia ubunifu unaolenga kuvutia watumiaji wapya, wakati ambapo masoko ya walaji yanaanza kurejea kwenye hali ya kawaida baada ya kuathiriwa kwa muda mrefu na janga la Covid-19.

"Mwaka 2022 tulitoa matokeo juu ya ukuaji endelevu wakati tukibuni, si tu katika kupata watumiaji wapya, lakini kwa ajili ya kuweka jukwaa lenye ufanisi kwa washirika wetu wa matangazo ya biashara. Katika mazingira yaliyoko, hii inamaanisha kushusha gharama za kufikia chapa za washirika wetu barani," anasema Karanu.

Aliongeza kuwa Mdundo ina umakini mkubwa kwenye upanuzi ndani ya bara la Afrika. "Afrika ina uwezo mkubwa kutokana na ukuaji wa haraka wa soko la kipato cha kati. Tunafanya kazi katika nchi zote za Afrika, na masoko yetu makuu ya kibiashara yakiwa Kenya, Tanzania na Nigeria, tunatazamia kupanua masilahi yetu ya kibiashara hadi Ghana na Uganda ifikapo 2022."

Ikiwa imezinduliwa mwaka 2013, Mdundo ni huduma ya muziki mtandaoni, inayowezesha watu kupakua bure mamilioni ya nyimbo kutoka Afrika na sehemu nyingine duniani. Watumiaji wa jukwaa hili wanaweza kupakua na kutiririsha muziki kihalali kutoka wavuti ya Mdundo na Android bure.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BENZEMA AMHOFIA HAALAND
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Karim Benzema mwenye umri wa miaka 34, ametaka kukutana na Rais wa Real Madrid, Florentino Perez, huku akihofia kuwa huenda akapoteza nafasi yake katika timu ikiwa mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, atahama msimu huu. ***(Onze)***

### RICE THAMANI JUU
KOCHA wa West Ham, David Moyes anafikiri, Declan Rice mwenye umri wa miaka 23, ana thamani ya zaidi ya pauni milioni 100, huku Manchester United, Chelsea na Manchester City zote zikihusishwa kutaka kumnunua kiungo huyo wa kati wa England. ***(Metro)***

### CHELSEA WAMKOSA SULE
KLABU ya Chelsea imepata pigo baada ya Niklas Sule mwenye umri wa miaka 26, kukubali kujiunga na Borussia Dortmund msimu wa majira ya joto wakati beki huyo wa Ujerumani atakapoondoka Bayern Munich. ***(Mirror)***

### NKUNKU AOTA MBAWA
ARSENAL wamekabiliwa na pingamizi katika harakati zao za kutaka kumsajili, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24, kutoka RB Leipzig. ***(Sky Sport)***

### UNITED YAMUUZA PEREIRA
KLABU ya Manchester United imekubali ada ya pauni milioni 12 kwa mauzo ya kudumu ya kiungo wa kati wa Brazil, Andreas Pereira mwenye umri wa miaka 26 kwenda Flamengo. ***(Universo,via Sun)***


### GARNER NA MATUMAINI
JAMES Garner ana matumaini ya kubaki Manchester United msimu ujao huku kiungo huyo mwenye umri wa miaka 20, akikaribia miezi ya mwisho ya muda wake wa mkopo kule Nottingham Forest. ***(Manchester Evening News)***

### TRAORE AUNGWA MKONO
KOCHA wa Wolves, Bruno Lage amemuunga mkono winga wa Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 26 kupata uhamisho wa kudumu wa pauni milioni 29 kwenda Barcelona. ***(Mirror)***

### BIELSA AITETEA LEEDS
KOCHA wa Leeds United, Marcelo Bielsa ameitetea klabu hiyo kutosajili mchezaji Januari na kuongeza kuwa hakupanga kufanya hivyo. ***(Mail)***

### GOSENS HAKUITAKA NEWCASTLE
MLINZI wa kushoto wa Ujerumani, Robin Gosens mwenye umri wa miaka 27, amesema alizingatia ofa kutoka Newcastle United kabla ya kuchagua kujiunga na Inter Milan kutoka Atalanta Januari. ***(Kicker)***

### SCOTT AWINDWA EVERTON
EVERTON na Leicester City, pamoja na klabu nyingine kadhaa za Ligi Kuu England, zinamfuatilia kiungo mshambuliaji wa Bristol City na England chini ya miaka 19, Alex Scott. ***(Football Insider)***



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AIBUKA, AKANA KUZUNGUMZA NA MADRID

Bado sijafanya maamuzi, ukweli ni kwamba, tunacheza dhidi yao, hilo linabadilisha mambo mengi...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amekanusha madai kwamba tayari amefikia makubaliano ya kujiunga na Real Madrid mwishoni mwa msimu huu.

Straika huyo wa Ujerumani alizungumzia majaliwa yake ya baadaye baada ya kuwa na wakati mzuri huku timu yake ikishinda mabao 5-1 dhidi ya Lille kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Jumapili.

Gazeti la Bild la Ujerumani hivi karibuni liliripoti kwamba, Mbappe na Madrid wamefikia makubaliano ambapo nyota huyo wa Ufaransa atatua pale Santiago Bernabeu mwishoni mwa msimu huu.

Mkataba wa sasa wa Mbappe na PSG unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, ingawa klabu yake ya PSG inapambana kuongeza mkataba wake.

Real Madrid haijaficha nia yake ya kutaka kumsajili Mbappe wakati wa kipindi cha usajili wa majira ya joto kinachokuja.

Mbappe mwenye umri wa miaka 23, atakuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu, lakini PSG imepangwa kucheza na Madrid kwenye hatua ya 16 bora ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Miamba hiyo ya Ulaya itakutana kwenye mchezo wa kwanza Februari 15, jijini Madrid na watarudiana Machi 9, mwaka huu, huku Mbappe akibainisha kwamba anataka kuisaidia timu yake kushinda taji hilo.

Alipoulizwa kama tayari ameshaamua majaliwa yake au mchezo dhidi ya Madrid unaweza kuchangia chaguo lake, Mbappe aliiambia Amazon Prime Sport Video: "Hapana, bado sijafanya maamuzi.

"Ukweli ni kwamba, tunacheza dhidi ya Real Madrid, hilo linabadilisha mambo mengi. Hata kama ninakuwa huru kufanya chochote kwa wakati huu, siwezi kwenda na kuzungumza na wapinzani wetu au kufanya lolote.

"Akili yangu kwa sasa ni kuisaidia timu yangu kushinda dhidi ya Real Madrid, kujaribu kuweka tofauti. Na baada ya hapo tutaangalia nini kitatokea."

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 918

MECHI KALI

AL HILAL RIYADH
VERSUS
CHELSEA

1 | 10.59
X | 5.97
2 | 1.19

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RANGNICK: SINA TATIZO NA LINGARD




**MANCHESTER, England**

KOCHA wa muda wa Klabu ya Manchester United, Ralf Rangnick, ameweka wazi kuwa hana tatizo na mchezaji wake, Jesse Lingard, baada ya kutofautiana maneno kuhusu kutojumuishwa kwenye kikosi wiki iliyopita katika mchezo wa FA dhidi ya Middlesbrough.

Man United walitupwa nje kwenye michuano hiyo kwa changamoto ya mikwaju ya penalti baada ya kutoshana nguvu kwenye muda wa kawaida.

Rangnick alisema kuwa Lingard alimuomba kupumzika baada ya kushindwa kufanikisha uhamisho wake wa mkopo kwenye dirisha la Janauri, lakini mchezaji mwenyewe alidai kuwa klabu ilimtaka apumzike.

Rangnick amejaribu kuweka sawa kwenye kikao na waandishi wa habari kabla ya mchezo wake wa jana Jumanne wa Ligi Kuu England dhidi ya Burney.

"Kuhusu Lingard, nina mahusiano naye mazuri tu, inabidi tuangalie mbele sasa," alisema Rangnick.

"Hakukuwa na tatizo lolote kati yangu na Jesse, nina furaha kuwa naye kwenye kikosi changu na atakuwapo kwenye wachezaji waliojumuishwa katika kikosi changu."

# Arsenal yashauriwa kuachana na Lacazette

**LONDON, England**

NYOTA wa zamani wa Klabu ya Arsenal, Paul Merson ameiambia timu yake hiyo kutompa mkataba mpya mshambuliaji wao, Alexandre Lacazette na kumuacha aondoke mwishoni mwa msimu ingawa yupo kwenye kiwango kizuri.

Mkataba wa mshambuliaji huyo unamalizika mwishoni mwa msimu huu wa majira ya joto na kwa sasa yupo huru kufanya makubaliano na klabu yeyote ile ikiwa atahitaji kufanya hivyo.


Merson ameionya klabu yake hiyo ya zamani ili yasitokee kama yaliyotokea kwa mshambuliaji mwenza, Pierre Aubameyang.

"Kama Lacazette akiendelea na kiwango hiki na akafanikiwa kufunga mabao 10 kabla ya msimu kuisha, Arsenal watapata uchizi na kumpa mkataba mpya wenye thamani ya pauni 250,000 kwa wiki.

"Arsenal wanachopaswa kufanya ni kuzuia, kisije kutokea kama kilichotokea miaka mingi iliyopita, ambapo walikuwa na vijana bora sana uwanjani, lakini ghafla unasikia kuna mkutano na tayari wameshaondoka.

"Hilo halipaswi kutokea, Arsenal inabidi waboreshe mikataba ya wachezaji wenye umri mdogo na wanawachezaji wazuri tu vijana.

"Arsenal hawawezi kubweteka tu kwa wachezaji ambao muda wao unafika mwishoni na kuwaacha vijana wanaondoka bure."



## HABARI MICHEZO


3,137,180

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/02/21 | 18:00 | Brentford vs Crystal Palace | 2.60 | 3.09 | 2.84 |
| 02. 12/02/21 | 18:00 | Peterborough vs Preston | 2.75 | 3.15 | 2.51 |
| 03. 12/02/21 | 18:00 | Reading vs Coventry | 2.79 | 3.19 | 2.45 |
| 04. 12/02/21 | 18:00 | Birmingham vs Luton Town | 2.81 | 3.15 | 2.46 |
| 05. 12/02/21 | 18:00 | Nottingham vs Stoke City | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 06. 12/02/21 | 18:15 | Villarreal vs Real Madrid | 2.74 | 3.32 | 2.54 |
| 07. 12/02/216 | 18:15 | Perugia vs Frosinone | 2.40 | 3.14 | 2.90 |
| 08. 12/02/21 | 20:00 | Napoli vs Inter | 2.81 | 3.41 | 2.44 |
| 09. 13/02/21 | 15:00 | Sheffield Wed vs Rotherham | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 10. 13/02/21 | 16:00 | Alaves vs Valencia | 3.04 | 3.24 | 2.36 |
| 11. 13/02/21 | 18:00 | Real Oviedo vs Huesca | 2.46 | 3.15 | 2.81 |
| 12. 13/02/21 | 19:00 | Kasimpasa vs Alanyaspor | 2.61 | 3.30 | 2.56 |
| 13. 13/02/21 | 19:30 | Leicester vs West Ham | 2.85 | 3.45 | 2.38 |

MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 09/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4419 | Bandirmaspor vs Sivasspor | 2.99 | 3.28 | 2.17 |
| 16:30 | 2644 | Sigma Olomouc vs Slovacko | 2.50 | 3.32 | 2.50 |
| 16:30 | 4959 | CF Monterrey vs Jazira Abu Dhabi | 1.31 | 4.63 | 8.29 |
| 17:00 | 4083 | Anagennisi Karditsas vs Panathinaikos | 4.81 | 3.47 | 1.66 |
| 17:30 | 1385 | Hatayspor vs Antalyaspor | 2.13 | 3.22 | 3.13 |
| 19:00 | 2123 | Olympiakos vs Panetolikos | 1.20 | 5.60 | 11.59 |
| 19:00 | 2312 | Bekescsabai Elore vs Gyirmot FC | 3.81 | 3.57 | 1.79 |
| 19:00 | 3621 | Csakvari TK vs Paksi FC | 6.17 | 5.21 | 1.34 |
| 19:00 | 5520 | KuPS Kuopio vs Seinajoen JK | 2.01 | 3.28 | 3.37 |
| 19:00 | 5924 | Slavia Prague vs Sparta Prague | 1.81 | 3.47 | 3.85 |
| 19:15 | 5116 | Kecskemeti TE vs Budapest Honved | 4.24 | 4.05 | 1.62 |
| 19:30 | 1649 | Olimpija Ljubljana vs NK Mura | 2.41 | 3.04 | 2.80 |
| 19:30 | 2764 | Al Hilal Riyadh vs Chelsea | 10.59 | 5.97 | 1.19 |
| 19:30 | 3274 | GKS Piast Gliwice vs Gornik Zabrze | 2.10 | 3.28 | 3.14 |
| 20:00 | 1331 | Paeek vs Apoel Nicosia | 9.35 | 4.97 | 1.31 |
| 20:30 | 4839 | Denizlispor vs Trabzonspor | 6.91 | 4.99 | 1.32 |
| 20:30 | 5405 | Bergerac Perigord FC vs FC Versailles 78 | 2.21 | 3.21 | 3.21 |
| 20:45 | 1897 | Zulte Waregem vs Oostende | 2.18 | 3.54 | 3.00 |
| 20:45 | 4219 | KVC Westerlo vs MSK Deinze | 1.94 | 3.56 | 3.46 |
| 20:55 | 3166 | Clinceni vs Steaua Bucuresti | 34.46 | 9.84 | 1.05 |
| 21:00 | 2889 | AEK Athens vs PAOK | 2.45 | 3.12 | 2.69 |
| 21:00 | 3978 | Waalwick vs AZ Alkmaar | 5.57 | 4.42 | 1.44 |
| 21:00 | 5915 | Ajax vs Vitesse Arnhem | 1.10 | 8.08 | 15.40 |
| 22:00 | 1815 | Vasas SC vs Ferencvaros TC | 5.39 | 4.24 | 1.47 |
| 22:00 | 5409 | Etoile Carouge FC vs St. Gallen | 5.97 | 4.72 | 1.39 |
| 22:30 | 1320 | FC Biel-Bienne vs FC Luzern | 5.41 | 4.54 | 1.44 |
| 22:45 | 1174 | Ross County vs Livingston | 2.32 | 3.26 | 2.96 |
| 22:45 | 1318 | Kilmarnock vs Ayr United | 1.72 | 3.62 | 4.40 |
| 22:45 | 1562 | Norwich City vs Crystal Palace | 3.44 | 3.34 | 2.13 |
| 22:45 | 1564 | Arbroath vs Hamilton | 1.91 | 3.47 | 3.67 |
| 22:45 | 1938 | St Mirren vs St Johnstone | 2.29 | 3.01 | 3.26 |
| 22:45 | 2041 | Preston vs Huddersfield | 2.13 | 3.25 | 3.30 |
| 22:45 | 2183 | Bournemouth vs Birmingham | 1.50 | 4.04 | 6.10 |
| 22:45 | 2360 | Tottenham vs Southampton | 1.61 | 4.09 | 5.19 |
| 22:45 | 2361 | Cardiff vs Peterborough | 1.83 | 3.58 | 3.92 |
| 22:45 | 2547 | Sheffield Utd vs West Bromwich | 2.33 | 3.20 | 2.95 |
| 22:45 | 2864 | Manchester City vs Brentford | 1.15 | 7.58 | 17.70 |
| 22:45 | 3137 | Bristol City vs Reading | 1.93 | 3.58 | 3.53 |
| 22:45 | 3218 | Rangers vs Hibernian | 1.30 | 5.15 | 9.11 |
| 22:45 | 3365 | Blackburn vs Nottingham | 2.28 | 3.14 | 3.09 |
| 22:45 | 4170 | Dundee Utd vs Motherwell | 2.38 | 3.16 | 2.96 |
| 22:45 | 4661 | Aberdeen vs Celtic | 5.73 | 4.05 | 1.53 |
| 22:45 | 4667 | Inverness vs Partick Thisle | 2.27 | 3.18 | 3.03 |
| 22:45 | 4921 | QPR vs Middlesbrough | 2.55 | 3.14 | 2.70 |
| 22:45 | 5936 | Hearts vs Dundee FC | 1.52 | 4.14 | 5.72 |
| 23:00 | 2192 | OH Leuven vs Racing Genk | 3.41 | 3.60 | 1.98 |
| 23:00 | 3857 | Aston Villa vs Leeds | 1.78 | 3.91 | 4.11 |
| 23:00 | 5467 | AC Milan vs Lazio | 1.80 | 3.76 | 3.95 |
| 23:00 | 5656 | Rayo Vallecano vs Betis | 2.75 | 3.20 | 2.51 |
| 23:15 | 5503 | Nice vs Marseille | 2.47 | 3.17 | 2.82 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# LUSAJO SASA MWIBA KWA MAYELE, KAGERE

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili yaliyofungwa na Reliants Lusajo kwenye Uwanja wa Ilulu Lindi Jumamosi iliyopita, akiibeba timu yake ya Namungo FC kushinda 3-1 dhidi ya Mtibwa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, yamemfanya kuzidi kuchanja mbuga kuelekea kutwaa Kiatu cha Dhahabu, akifikisha mabao tisa mpaka sasa.

Wakati ikisalia raundi moja tu kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, straika huyo Mtanzania amekuwa kwenye kiwango cha juu msimu huu, ambapo mbali na kufunga mabao hayo mawili, pia ndiye aliyetoa nafasi ya bao moja.

Mabao yake tisa, yamemfanya kuzidi kuwatimulia vumbi mastraika wa timu kubwa nchini; Simba na Yanga ambao wanaimbwa na mashabiki wengi, Fiston Mayele wa Yanga na Meddie Kagere wa Simba.

Straika huyo ametanua wigo kwa wanaomfuatia, kwani amewazidi wanaomfuata kwa tofauti ya mabao matatu nao ni Mkongomani Mayele ambaye ana mabao sita, na wengine wenye idadi hiyo ya mabao ni George Mpole wa Geita Gold, na Vitalis Mayanga wa Polisi Tanzania.

Mnyarwanda Kagere wa Simba mpaka sasa amepachika mabao matano, huku Jeremiah Juma wa Prisons naye akiwa na idadi.

Wachezaji ambao wana mabao manne mpaka sasa ni Richardson Ng'ondya na Juma Luzio wote wa Mbeya City, Feisal Salum wa Yanga na Rodgers Kola wa Azam FC.

# Medo atangaza vita ya pointi Coastal



Melis Medo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Melis Medo, ametangaza vita kali kwa wapinzani wao katika michezo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Melis alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa na kwamba watahakikisha wanashinda mechi zote zilizobaki ili kupanda katika nafasi tano za juu.

Alisema katika michezo minne iliyopita ya ligi ambayo wamecheza wamepoteza, hali ambayo inaonyesha dhahiri kuna upepo mbaya unaowakumba tofauti na mwanzo wa msimu huu.

"Tunaenda kupambana na upepo huu mbaya uliokumba timu yetu, tukianzia mechi ya mwisho ya mzunguko wa kwanza kutafuta matokeo mazuri ambayo itakuwa mwanzo mzuri wa raundi ya pili itakayoanza hivi karibuni," alisema Melis.

Alisema hawako sehemu mbaya wala nzuri kwa sababu wamepishana pointi chache na walioko juu yao, wakiwa nafasi ya tisa kwa pointi 17 sawa na Polisi Tanzania waliopo nafasi ya nane.

"Ukiangalia msimamo wa timu zimepishana pointi chache sana, vita ndio kwanza inaanza maana tumebaki na mchezo mmoja kabla ya kuelekea mzunguko wa pili ambao huwa ni mgumu zaidi na kuhakikisha tunashinda ili kufikia malengo yetu," alisema Melis.

Coastal Union iko nafasi ya tisa ikiwa na pointi 17 kwa michezo 14 iliyocheza, na imetoka kupoteza hivi karibuni mechi nne mfululizo baada ya kuanza kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, ikafungwa mabao 2-0 na Yanga, kisha wakapigwa 3-1na Namungo FC kabla ya kulazimika kula kichapo kingine cha 2-1dhidi ya Kagera Sugar.

Michezo
Jumatano Februari 9, 2022
Nipashe



**Mbappe aibuka, akana kuzungumza na Madrid**

ACHENI WAJE...



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini. Jumapili watashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Asec Mimosas kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: MAKTABA**

# SIMBA KUTOA MAKUCHA KWA ASEC MIMOSAS CAF

●●●Yaita mashabiki kuona mechi ya maana kwa buku tano tu, yasema huwa huifanyi makosa...

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Simba imetamba kuwa itaonyesha 'makucha' yake kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho la Afrika (CAF), kwa kucheza kikubwa tofauti na inavyocheza michezo ya Ligi Kuu Tanzania, huku ikificha siri ya shirikisho hilo kuwaruhusu kuingiza mashabiki 35,000 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Simba ambao ni wawakilishi pekee kwenye michuano ya kimataifa, Jumapili wiki hii itajitupa kwenye uwanja huo, kucheza mechi ya kwanza ya makundi ya michuano hiyo dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, akizungumza jijini Dar es Salaam, alisema hizo ndizo mechi ambazo timu yao hupenda kucheza na mashabiki wao wanapenda kuzitazama kwa sababu hakuna 'kupaki basi.'

"Hizi ndiyo aina ya mechi ambazo Simba inapenda kucheza, na ndiyo aina ya michezo ambayo 'tunainjoi' tukicheza, na mashabiki wetu nao wanapenda kuzitazama kwa sababu hizi siyo zile mechi ambazo mwamuzi anapuliza kipenga tu, basi wachezaji wote wanarudi nyuma, hii si aina ya michezo ambayo timu yetu inapenda kucheza.

"Halafu makipa muda mrefu wanakuwa wakipoteza muda, kwenye mechi hizi za Kombe la Shirikisho huwezi kucheza kwenye uwanja kama wa Manungu Complex, au kupaki basi, tunakwenda kucheza na timu ambazo tunapishana nazo, inaweza kuwa ngumu kucheza na Prisons, lakini ikawa rahisi kucheza dhidi ya RS Berkane kwa sababu huko tunacheza kikubwa na mechi ya Jumapili tunacheza kikubwa," alisema Meneja habari huyo.

Kuhusu kuruhusiwa mashabiki 35,000, alisema CAF huwa hairuhusu timu hivi hivi kuingiza watazamaji na ndiyo maana mechi za awali za kimataifa timu zote ikiwamo Yanga, Azam na Biashara United hazikuruhusiwa kufanya hivyo zaidi ya Simba tu.

"Tunawashukuru CAF kwa kuturuhusu kuingiza mashabiki 35,000, haijaja kwa bahati mbaya, tuna janga la COVID-19, ili uruhusiwe kuingiza mashabiki kuna vigezo. Tuliona kule mwanzo timu nyingine hazikuruhusiwa kuingiza mashabiki, Simba iliruhusiwa kwa sababu CAF inafahamu uongozi wa Simba unafuata masharti ambayo CAF wanayoyatoa kwa sababu imeshiriki mara kwa mara michuano hiyo na imetekeleza kwa hiyo ilikuwa na imani na sisi.

"Pia mashabiki wa Simba kwa sababu ni wazoefu wa kuingia uwanjani kwenye michuano ya kimataifa, CAF wakaona ni rahisi kutekeleza masharti hayo, kuliko timu ambazo ni wageni wa michuano hiyo, hasa kwenye kipindi hiki cha COVID-19," alisema.

Kwa upande wa Meneja wa klabu hiyo, Patrick Rweyemamu, amesema kikosi kinaendelea vizuri na mazoezi kuhakikisha wanapata pointi tatu kwenye mchezo wao wa wikiendi hii dhidi ya miamba hiyo ya Ivory Coast.

Meneja huyo alisema mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani, hivyo akawataka mashabiki na Watanzania kwa ujumla kujitokeza kwa wingi uwanjani kuisapoti timu yao.

"Tunaomba mashabiki waje kwa wingi uwanjani kuiunga mkono timu yetu ambayo ni mshiriki pekee ambaye anashiriki mashindano ya kimataifa," alisema.

Katika hatua nyingine klabu hiyo imetangaza viingilio katika mechi hiyo kuwa ni Sh. 5,000 kwa Mzunguko, Sh. 20,000 kwa VIP B na C, huku VIP A ikiwa ni Sh. 40,000 tu.

## Yanga waanza kulia na waamuzi

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umesema hauridhishwi na mwenendo wa waamuzi wanaochezesha michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, wakati huu wakiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa pointi tano zaidi ya watani zao, Simba wenye alama 31 katika nafasi ya pili.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema licha ya kuongoza ligi kwa pointi tano, lakini hawaridhishwi na mwenendo wa waamuzi wanaochezesha Ligi Kuu na kwamba wameshuhudia matukio kadhaa ya kusikitisha kwa waamuzi kuyafanya katika baadhi ya mechi na kufaidika kwa timu moja.

"Tunazitaka mamlaka zinazosimamia soka kuchukua hatua juu ya maamuzi ya waamuzi kwa yanayoendelea ili kuwe na thamani ya ligi yetu kama sasa hivi inavyodai ipo nafasi ya 10 kwa ubora Afrika," alisema Bumbuli.

Wakati Bumbuli akisema hayo Msemaji wa Yanga, Haji Manara, amelitaka Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kuchukua hatua sawa kwa viongozi wote bila kujali ukubwa wa timu.

Alisema anastaajabu kuona viongozi wa Simba kutochukuliwa hatua baada ya kudai kwamba TFF na Bodi ya Ligi Tanzania kuambiwa wamewaandaa Yanga kuwa mabingwa.

"Kuna viongozi wa Yanga akiwamo Fredrick Mwakalebela na Bumbuli walifungiwa hapa na faini ya fedha nyingi kuliko viongozi wa Simba, hapa wamepewa adhabu ya faini ya laki tano, kwa kutoa kauli ya kwamba TFF na Bodi inapanga Yanga kuwa bingwa.

"Hii inaonyesha kwamba watu (Simba) wanaogopwa, hatulalamiki, tunaweka kumbukumbu sawa, makosa yanayofanywa na viongozi basi wanatakiwa kuadhibiwa kwa stahili ya makosa wanayostahili," alisema Manara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >